Maswali na Majibu

Na tuendelee kusimama kidogo tu kwa ajili ya maombi.

Mungu mpendwa, tunakushukuru usiku huu kwa ajili ya, kwanza, kwa ajili ya Yesu Kristo, Mwokozi wetu. Tunakushukuru kwa sababu ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunakushukuru kwa ajili ya watu wanaoamini hayo. Tuna furaha sasa kuwa tuna Mungu, si Mungu wa kuwazia tu, sanamu ya kuwazia, roho wa kuwazia; hakuna cho chote cha kuwazia juu yake—Mungu wa Kweli na aliye hai ambaye huishi pamoja nasi na kati yetu na hutenda kazi kwetu. Si kumfanyia Mungu sanamu, bali sisi tukiwa mifano iliyo hai ya Mungu... Roho Mtakatifu, si akinena kupitia kwa sanamu, bali akinena kupitia kwa chombo kilichokombolewa—Mungu akidhihirishwa katika mwili. Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya hii, ile Nguzo kuu ya Moto ikitufuata, ama sisi tukiifuata, nakusudia, na kwa dhihirisho zote kuu za Roho yule yule akitenda kazi ile ile ambayo ameitenda kila mara alipokuja ulimwenguni. Jinsi inavyotufariji sisi.

2 Tumekusanyika hapa usiku huu, Bwana, si kwa kusudi lingine ila kujua na kujifunza, kwa msaada Wako, jinsi ya kuwa Wakristo bora na raia bora wanaostahili kwa ajili ya wakati huu tunaouendea. Si utatusaidia, Bwana; tunakuhitaji Wewe. Katika Jina la Yesu. Amina. (Mwaweza kuketi).

3 Yalikuwa karibu maswali mengine thelathini au arobaini. Si—sijui jinsi ningeyafikia. Nimejaribu sana adhuhuri ya leo kuona kama ningeyafikisha wastani, lakini singeweza kufanya hivyo. Lakini ninataka kusema kuwa nitafanya kadiri niwezavyo ku—kujibu maswali haya, kwa sababu ni maswali mazuri, yanatoka mioyoni mwa Wakristo. Nami—nami hakika nataka kufanya kila niwezacho kuyajibu kwa busara tu nijuavyo kuyajibu. Na—nami nataka kumshukuru Bwana kwa jinsi ametusaidia asubuhi hii ku—kupata maswali haya na kuna ku—majibu, alitupea sisi.

4 Sasa, nimeyaweka hapa yote yamechanganyikana, nadhani 150 zaidi. Nasi tulifikia karibu ishirini, nadhani, asubuhi hii. Na—na kwa hivyo sasa, kabla hatujaanza, ningependa kusema sasa kwamba kama ye yote alitaka kuona nakala hii juu ya *Kanisa Lacheza Dansi Huku Ngoma Zikilia*, mhudumu wa Presbiteria hapa akiongoza kusanyiko lake katika rumba, mpango wa—wa sakramenti... Hebu nione kwa muda mfupi.

5 "Washiriki vijana wasakata muziki wa ngo—ngoma. Mchezo wa kuigiza waonyesha yale mateso ya Msalabani katika n-a-h-a-u ya kisasa, dansi ya rumba." Mchungaji yule hapa akiongoza vijana wote matineja juu pale wakionyesha mateso ya Kristo,

kule kusulubiwa kukichezwa katika rumba na bendi ya ngoma. Vema . . . Ni kule Maryland. Sasa, si hilo ni jambo fulani?

6 Halafu, hapa kuna picha ya wale . . . Nilikuwa nawaambia ninyi asubuhi hii juu ya wale Beatles, *Kurudi kwa Beatles*, na kuna nakala; inawapasa ninyi kusoma gazetini na mambo mengine mbalimbali. " . . . ni kama kwamba, wameanzisha dini mpya." Sasa, msimamizi wao . . . Nina kato la gazeti hapa. Hamna wakati . . . Kama ye yote anataka kusoma haya—au naweza kuyaweka kwenye ubao wa matangazo, ndipo mnaweza kuyasoma. Nami nataka tu kuwaonyesha ninyi wakati tunaoishi ni wa kutisha. Huenda msilielewe, lakini, enyi watu, jaribuni kufahamu haya, vile mambo haya ni nini! Nimemwuliza Ndugu Capps—yeye ana elimu nzuri na anaweza kusoma vizuri kuliko mimi—nimemwuliza yeye asome nakala hii toka kwa msimamizi wa Beatles. Waweza kuisoma, Ndugu Capps, wakati huu?

7 [Ndugu Caaps asoma nakala ya Beatles—Mh.] Inasema kuwa:

> Beatles wanashangaa kuhusu wao wenyewe na hawapati jawabu. "Haiaminiki, haiaminiki kabisa!" asema Derek Taylor, yule afisa mweneza habari wa Beatles, "Hapa kuna hawa wavulana wanne toka Liverpool. Wao ni wajeuri, ni makafiri, hawana adabu, nao wameuteka ulimwengu. Ni kama kwamba wameanzisha dini mpya. Wao ni wapinga Kristo kabisa. Naam, mimi pia ni mpinga Kristo; lakini wao ni wapinga Kristo mno hata wananishangaza mimi, ambalo si jambo rahisi. Lakini nimepagawa nao. Si ndivyo alivyo kila mtu? Nimepagawa na uaminifu wao na watu wanaowapenda sana ndio wale watu wanaopaswa kughadhabika zaidi."
>
> "Kule Australia, kwa mfano, kila wakati tulipowasili katika uwanja wa ndege, ilikuwa kama kwamba De Gaule alikuwa amewasili, au bora zaidi, Masihi. Barabara zilijaa kabisa. Viwete walitupa mikongojo yao. Wagonjwa walikimbia kwenye motokaa, kama kwamba mguso mdogo wa wavulana hawa ungewapa afya tena. Wanawake wakongwe na wajukuu wao walisimama wakitazama tulipokuwa tukipita. Ningeona mtazamo kwenye nyuso zao. Ilikuwa kama kwamba mwokozi fulani alikuwa amewawasili na watu hawa wote walikuwa na furaha na wamefarijika, kama kwamba kwa njia fulani mambo yatakuwa mema sasa." Taylor akatulia na akaweka sigara kinywani mwake, "Jambo pekee lililosalia kwa Beatles," yeye kasema, "ni kufanya safari ya uponyaji."

8 Si hayo ndiyo Yeye alisema? "Wengi watakuja Kwangu katika siku hiyo na kusema, 'Bwana si nime . . .'" Ona? Sasa, hamwezi kuona kuwa huwezi kuweka imani yako katika mikutano ya uponyaji? Huwezi kuweka imani yako katika aina

yo yote ya ishara hivyo. Jambo pekee unaloweza kuweka tumaini lako kwalo ni BWANA ASEMA HIVI toka kwa Biblia. Sasa, Kanisa, hapo ndipo hasa nimejaribu kuwaweka ninyi, watoto wangu. Na kama kitu fulani kikitendeka kwangu na Mungu aniondoe duniani humu, msishindwe kamwe. Kumbukeni hili kwa mioyo yenu yote: dumuni kwa Neno hilo! Msiache Neno hilo! Cho chote ambacho ni kinyume cha Hilo, kiachilie, haidhuru ni nini. Ndipo unajua ni sahihi. Ona?

9 Mkutano wa uponyaji sasa! Watu wenye dhambi mno hata wanamshutua msimamizi wao kwa utovu wao wa adabu, uchafu, na uovu; na watu wanatupa mikongojo yao na wanapona kwa kuwatazama wavulana hao. Ni chafu mno, na najisi, na pinga Kristo! Mwaona, ni Shetani akienda kwa mikutano ya kufanya mizaha. Ona? Yeye afanya lo lote ambalo Kristo aweza kufanya, lakini yeye hawezi kuthibitisha Neno. Ona? Yeye atachukua sehemu yake hapa na sehemu yake hapa, lakini yeye hawezi kulichukua lote pamoja. Ona? Yeye hawezi kulichukua lote pamoja. Kwa hivyo mwaona, si ajabu Biblia ilisema kwamba karibu lingepumbaza walio Wateule kama yamkini—yule roho mpinga Kristo.

10 Sasa, hata msimamizi wao mweneza habari hapa, mtangazaji wao, yeye anawaunga mkono, anawaamini, na kasema yeye amepagawa na kitu kile kile, kwa sababu wamemteka.

11 Hayo mambo maovu, hayo. . .Sasa, hamwoni, wanawake, jinsi ninavyojaribu kuwaambia ninyi kuhusu huu uvaaji wa suruali fupi, kukata nywele, kuzifupisha, na mengineyo. Ni pepo fulani. Ni pepo fulani! Iko papa hapa katika magazeti yetu makuu na kila kitu cha yale yanayoonyeshwa waziwazi—rumba na upuzi huo kanisani. Naam, ni mtego wa Shetani hasa, nayo bado yangali makanisa na madhehebu.

12 Rudini kwa Neno, watoto, upesi mjuavyo; na msithubutu kuliacha! Kaeni moja kwa moja na Neno hilo.

Ona, jinsi huyo roho mpinga Kristo, anaweza kunena kwa lugha, aweza kuonyesha ishara na maajabu; anaweza kuponya wagonjwa, anaweza kufanya mambo haya yote. Ona? Watu wale wakidhani wanamwendea Mungu, kuwa wavulana wale wametumwa na Mungu, kwa sababu kanisa limelegeza Neno.

13 Wavulana wale ni wa kanisa. Elvis Presley ni Mpentekoste. Pat Boone ni wa Church of Christ. Watazame wahuni hawa, Wapentekoste, Church of Christ, na kadhalika wakiwa na pepo wachafu juu yao. Red Foley, sauti ya dhahabu, Church of Christ, anaimba nyimbo za kidini kuliko ye yote awezavyo kuziimba na rumba katika sauti inayofuata. Kwa matunda yao mnawajua. Tazama wao ni wa makanisa gani. Elvis Presley ni washiriki wa Assemblies of God. Naam, kila mmoja wao alitaka hilo, na Shetani akawapa.

14 Hamwoni, marafiki, jinsi . . . Msilegeze Neno hilo. Ona, ni pepo anayekuingilia.

15 Nami nawaambia wanawake hawa, wanapojifanya wenyewe waonekane wazinifu katika mavazi haya, ya kwamba Mungu atawahukumu kwa kuzini. Kama mnaniamini mimi kuwa yale mnayosema, mtumishi wa Mungu, nabii, sikizeni yale ninayowaambia. Ona? Huenda msifahamu, na msipoweza, basi fanyeni tu yale ninayowaambia mfanye. Mungu atanihukumu kwa yale ninayosema. Ona? Sikizeni kwa makini sana, na kumbukeni kuwa vitu hivyo ni pepo.

16 Kwa kawaida, huenda ikawa mtu yule . . . Kumbukeni, *Mungu aliyefunikwa kwa ngozi*, nilihubiri hayo si muda mrefu uliopita (ona, ona?)—Mungu aliyevalia ngozi? Sasa, kumbukeni tu, wengine wetu tumetumwa ulimwenguni humu kuingia katika mazingara haya kutwambia mambo haya. Ona? Ni kufahamu tangu awali; ni Mungu akinena, akionyesha. Unapohukumu lo lote kwa mwili, naam, hawana hatia (tazama hapa), watu wazuri, waaminifu, hawangekwambia uongo wala cho chote kile. Na jambo lote ni Shetani. Wa kidini, hata kuanzisha mkutano wa uponyaji. Ona? Wa upinga Kristo kabisa. Ona? Na kuna Wapresbiteria na hayo wote. Mwayaona hayo madhehebu, jinsi wanavyofanya—katika kitu kile kile?

17 Naam, hapa London, Uingereza, hivi majuzi walikuwa na kundi la rumba kumuiga Kristo, na Yuda, na hayo yote, na . . . Walimwita Kristo "Baba-ee" na kunena maneno hayo yote wanayoongea watoto wenye wazimu. Ona? Vijana matineja waliuteka ulimwengu. Sasa, mwajua kuwa Biblia inatabiri hayo: Wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiopenda kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiotii wazazi wao (ona?), vijana matineja wakiuteka ulimwengu, na imetendeka.

18 Nilienda mahali fulani majuzi; walikuwa wakicheza hizi—mojawapo wa maskini hizi gramafoni chafu zinazocheza kwa pesa, upuzi huo wote. Hata sikutaka kuingiza jamaa yangu, Nilimwuliza mwanamke yule, "Santuri hizo zinagharimu nini?"

"Senti kumi kila upande."

"Itacheza ngapi kwa saa." Yeye aliniambia. Nilisema, "Fedha hizi; izime!"

"Vema," yeye alisema, "Singefanya hilo. Watoto hao huja hapa kuzicheza."

19 Ndipo singetumia pesa zo zote pale; nikaenda mahali pengine. Ona? Vema, upuzi huo ungekupa wasiwasi; ungepaswa kwenda ukanunua madawa ya kutuliza fahamu ukayameze baada ya kusikia wazimu huo. Hilo humchosha Mkristo. Kama unapenda upuzi wa aina hiyo, unajua una kasoro gani? Unahitaji kuokoka, kwa sababu kile kilicho ndani yako kinakula kitu fulani mbali na Neno. Kinakula . . .

20 Hungewaza Yesu akifanya jambo kama hilo, sivyo? Je, waweza kuwazia mmoja wa manabii akifanya kitu kama hicho? Hamwoni, marafiki, jambo hilo lote kila mahali ni shetani. Na Biblia ilisema jinsi yeye angeingia katika mfano wa dini na kufanya vivyo hivyo kama Kristo. Ona? Lakini njia pekee ambayo ungeweza kulitambua, si kujiunga na kanisa hili, au kujiunga na kanisa *hilo*, ni kukaa na Neno; Yeye ni Neno.

21 Sasa, Bwana abariki kila mmoja wenu. Tutaingilia yale maswali moja kwa moja. Na sasa, kwa karibu—hadi karibu saa moja na dakika kumi na tano . . . Sitaweza kumaliza maswali haya yote. Kunayo chungu nzima. Nafikiri ni maswali mazuri. Ni mazuri sana. Nitanyosha mkono na kuchukua moja hapa na pale ninapoendelea. Na sasa . . . kulijibu . . .

Ninge—nilidhani usiku huu ningekuja, niache mtu fulani ayasome, niseme, "ndiyo" au "La," "ndiyo" au "la" kwa . . . Hiyo si kuwafanyia watu haki. Wanauliza maswali hayo yapate kujibiwa. Nami—singefanya hivyo, kwa sababu nitachukua yale niwezayo, na yale siwezi, nitayapata wakati mwingine.

22 Na sasa, ni—ni . . . Yapata Jumapili inayokuja, sijui. Nawaambia; mkimwona Billy wakati fulani kati ya sasa na Jumatano . . . Huenda ikatubidi kuondoka.

23 Sasa, hapa kuna jambo moja. Nimechelewa kwa mahojiano. Billy alinionyesha kundi la mahojiano urefu *huu*, ambayo yamekuwa yakingoja. Wengine wao, kwa miezi kadhaa. Vema, niwapo humu, yanipasa nifanye baadhi ya hayo, kufanya baadhi ya mikutano hiyo, kufanya kila kitu niwezacho nipate kusawazisha. Ninaenda kuomba juma hili nitakapoondoka na kumsihi Bwana, "Ungependa mimi nifanye nini, kumaliza haya au—au kuchukua mahojiano?" Nikichukua mahojiano, basi nitakimbia—nitakuja nyumbani Jumapili na kuendelea na mahojiano moja kwa moja kufikia mahali fulani, na kuendelea kwa siku nzima na mahojiano. Na nisipofanya hivyo, naam, nitaahirisha mahojiano hata nitakaporudi tena. Nisipofanya hivyo, basi nitajibu . . . Nita . . . Billy atawatumia kadi.

24 Nami nawaambieni; ni vema, hawa watoto wapendwa, kuwaambieni jinsi hawa wanavyopendana, upendo ule walio nao wao kwa wao. Mmoja atamwambia mwingine na mwingine atamwambia . . . Billy humpigia simu mmoja katika sehemu fulani, mmoja karibu maili mia na hamsini, na wengine wao huwapasha wengine wao. Wanapendana. Hawataki kukosa cho chote. Wana—wanataka kuwa hapa kila dakika kuona yale yanayoendelea; kwa maana kama Bwana akitoa kitu fulani, wanataka kuwa hapa kukipokea. Nami nawapenda.

25 Sasa kumbukeni, marafiki wapendwa, asubuhi hii nilitoa matamshi kwa maswali fulani. Nami natambua baadhi ya haya (naam!) hali—yaliingia asubuhi hii, zaidi sana ni kuhusu watu

kuhamia Arizona. Ona? Nilidhani ninge—heri nilifanye dhahiri, ili mfahamu.

26 Sasa, msi—msidhani kwamba ninajaribu kuwaambia watu mahali ambapo wanaweza kuishi, na kile wanachoweza kufanya, na . . . Sasa, ninasema hayo, ndugu yangu mpendwa. Kuna watu waaminifu wanaotaka kuhamia . . . Vema, mtu ye yote anayetaka kuhama, hakika ni—ningefurahi, mradi tu niko kule ambalo—mradi tu niko kule . . . Niko hapa karibu mara kumi nilivyo kule. Nina . . . Kati ya sasa na Krismasi, nina karibu siku nne kuwa kule. Ndipo mara tu baada ya hayo, ninaenda ng’ambo. Nitakuwa hapa maskanini labda majuma mawili au matatu kabla sijaenda ng’ambo kwa—kwa ufufuo, kama nifanyavyo haya majira ya katikati ya mwako. Na ndipo toka pale, nina mkutano mmoja tu katika Arizona yote, nao utaanza Januari kule Phoenix, jioni mbili pamoja na Wafanyi Biashara Wakristo. Ona? Mimi si . . . kama watu kule nje . . . Waweza kuzima kile kinasa sauti? [Ndugu Branham aomba kwamba kanda zizimwe na kuongea na kusanyiko—Mh.]

27 Sasa tunapoanza maswali haya usiku huu, nitachukua moja hapa na . . . Je, mnayafurahia? Semeni, “Amina!” [Makutano wajibu, “Amina!”—Mh.] Nadhani ina manufaa kwetu wakati huu. Basi ee, naamini hivi punde kwa . . . Nikitazama asubuhi hii kabla sijakuja hapa baadhi—mafungu fulani na mahali fulani katika Biblia, nilifikiri, “Ee, lingekuwa ni jambo la ajabu jinsi gani . . . Tunapongoja kule kuja kwa Bwana, lingekuwa jambo la ajabu jinsi gani kurudi nyuma katika hao watu wote wa Agano la Kale, kupitia Ayubu na kupitia pale, na kuendesha mfululizo wa mikutano juu yao (si hilo lingekuwa ajabu?), kuwaonyesha ninyi tu jinsi yanavyotoa mfano mpaka siku hii (Neno lote linafungamanika pamoja), na yote kuhusu uharibifu wa—wa wakati wa kale na jinsi vinavyotoa mfano wa siku hizi; jinsi kila kitu katika Agano la Kale kinanena kuhusu kule kuja kwa Bwana Yesu.

279. Sasa, swali la kwanza nililovuta toka hapa; **Ndugu Branham, ni kosa kwa Mkristo kuweka—kuweka kwa nywele zake vipini vya kusokota? Pia, mikono ya nguo yake yapaswa kuwa urefu gani? Asante. Dada fulani.**

28 Sasa, hilo—lina maana kubwa sana kwa mwanamke huyo. Sasa, kwa wengine wa ndugu zetu huenda sisi tukadhani, “Ee, huyo mwanamke mpumbavu.” Lakini—lakini si upumbavu kwake; yeye ataka kujua.

Sasa, kuhusu kuweka nywele kwa kile mlikiitaje, kusokota kisogoni au kitu gani? Ninasikitika. Si—mimi si- . . . Ili- . . . Nasikitika. Kusokota kwa vipini. Kunradhi. Kundi la vipini—kusokota nywele kisogoni! Hivyo ndivyo wasichana walikuwa wakivalia miaka mingi iliyopita. Mnakumbuka, namna . . .

Sivyo? Waliviita kusokota kisogoni, imesokotwa tu kuning'inia chini? La, misokoto ya vipini, kunradhi, rafiki.

29 "Avae nguo zenye mikono urefu gani?" Sasa, sidhani hiyo ni kitu. Sijui. Ona? Yale siwezi kuthibitisha kwa Biblia, si—sitaki kusema mengi juu yake.

30 Sasa, nawambia hili tu kwa ajili yangu, kwa sababu sina Andiko la kuliunga mkono. Jambo pekee nililo nalo kwa kina mama kuhusu nywele zao ni zisikatwe. Jinsi wanavyotaka kuitengeneza, hilo ni juu yao. Na kuhusu kusokotwa kwa vipini, kweli, sijui hivyo ni nini, isipokuwa viwe ni vitu hivi vinavyoonekana kama visindano vya nguo wanavyoviweka katika nywele zao. Kama ni . . . jambo pekee ninalojua . . .

31 Na urefu wa mikono ya nguo, nadhani, ukiwa Mkristo, Mungu angekwambia la kufanya kuhusu mambo hayo. Mwaona? Naamini kama mtu Mkristo unge—ungejua jinsi ya kufanya hili. Sidhani Mungu hukata urefu wo wote au cho chote kile. Mradi tu umevalia ifaavyo na unaonekana mzuri na msafi, ni—ninadhani hilo ni sawa. Sivyo? Sasa, hilo ni wazo langu tu. Sasa, hili ni mimi, ona, kwa sababu siwezi kuthibitisha lingine lo lote kwa Andiko.

32 Naamini asubuhi hii swali lilikuja kuhusu kupaka nywele rangi, mwajua, na—na rangi. Sasa, si—si—ni si—siwezi kusema lo lote kuhusu hilo. Sijui, lakini si—si—sina Andiko kusema msi—msitie nywele rangi. Sasa, hilo ni—hilo ni . . .

Ninyi wanawake, mnapenda kuonekana wazuri, na yapasa mwonekane wazuri. Na Ndugu Branham hayuko dhidi yenu watoto. Ninyi ni watoto wangu; ni—ni—ninawapenda ninyi, na si—sitaki kuwakemea. Si—singelifanya hivyo bila sababu; ninajaribu tu kuwasaidia.

33 Lakini sasa, tazama, hebu tu niulize . . . Hebu niseme hili kama jibu kwa swali hilo. Sasa, mko tayari? Na kwenu mlio kwenye kanda, ni hivi basi, akina dada: Kama kuna swali ndani yake, usilifanye. Lakini kama ume—kama umejazwa na Roho wa Mungu na unaongozwa kuenda kulifanya, mradi tu haliingilii Maandiko na halizushi swali, umeridhika kabisa kuwa hayo ni mapenzi ya Bwana, basi nenda kafanye vile (ona?), kwa sababu hakuna Andiko linalosema la (ona?) kulihusu. Si . . . Haisemi cho chote kama hicho katika Biblia.

34 Najua Isaya 5, naamini ndiyo, ilinena kuhusu wanawake, jinsi watavalia mavazi yanayobadilika na kadhalika; lakini hayo yalikuwa majivuno na kadhalika, mapambo. Ukifanya hivyo kwa kujionyesha, basi ni kosa. Ona? Jichunguze moyo wako mbele za Mungu. Kama hakuna Andiko kwa hilo, na jinsi Roho akuongozavyo, basi fanya hivyo. Lakini sasa inapofikia kama yakupasa kuwa na nywele ndefu au nywele fupi, wewe kuwa na nywele ndefu; hiyo ni Biblia.

35 Kuna swali hapa; hu—huenda nitalijibu sasa hivi. Liko ndani humu; nililiona asubuhi hii au wakati fulani. Kasema, "Wewe kila siku unanena kuhusu wanawake, jinsi hawapaswi kuweka nywele zao, lakini huneni lo lote kamwe kuhusu wanaume."

36 Kama nikimwona mwanamume akiingia humu akiwa na nywele ndefu zikining'inia mgongoni mwake kama mwanamke, ningesema, "Bwana, mbona usiende kwa kinyozi? Unaonekana kama mwanamke." Ona? Lakini wanaume kwa kawaida hawafanyi hivyo. Ona? Si kama wanaume . . . Sasa, si kusema wanaume hawakosei, wao wana hatia tu kama wanawake.

Na katika hili, mwanamume atakayeacha mke wake afanye hivyo, yeye ana hatia maradufu ya hilo, kwa sababu yeye anapaswa kuwa ndiye aliye na mamlaka nyumbani. Na mwanamume ambaye hata hawezi kuitawala nyumba yake; angewezaje kufanya hivyo katika nyumba ya Mungu? Ona?

37 Nina shukrani sana kwa ajili ya kundi letu la wanawake wanaokuja hapa. Nasema hili kwa heshima na upendo, na sasa, Mungu ajua hili ni kweli. Ni—nilikuwa na rafiki mhubiri kule chini Kusini aliyekuwa na mojawapo wa makanisa masafi sana niliyowahi kuona. Ifikiapo kwa wanawake, wanawake warembo sana niliowahi kuona waliketi pale kitakatifu, kitauwa, wakiwa na nywele ndefu. Nami kila siku nilipenda kuhudhuria kanisa hilo. Na Bwana Yesu amenipa kanisa leo hapa ambalo linang'aa kushinda hilo maili mia—wanawake wangu.

38 Siwakaripii ninyi iii niwe mbaya; nina furaha nyingi kwa ajili yenu. Sitaki tu Shetani aingize mguu wake po pote. Ona? Nataka ninyi mwelekee juu, si nyuma. Msiache mtu ye yote awadanganye ninyi kwa hila fulani, au kitu kama hicho, au jambo fulani akisema, "Lo, vema, haimaanishi . . . " Ona? Hivyo ndivyo Shetani alivyomfasiria Hawa Neno. Ona? Aminini tu yale Neno lisemayo. Vema.

280. Haraka sana. Ndugu Branham, tukijua kuwa wakati unakwisha na milele inaingia, ungewashauri vipi mvulana na msichana wanaopanga kuoana?

39 Endeleeni mkaoane. Endeleeni tu kama kwamba mtaishi miaka mingine mia moja hapa duniani. Endeleeni tu; elekeza moyo wako kwa Kristo, si mioyo yenu kwa mambo yaliyo ulimwenguni, lakini kwa Kristo. Ona? Endeleeni; oaneni, enyi watoto. Mungu awabariki katika arusi yenu.

281. Mpendwa Ndugu Branham, nimebatizwa katika Jina la Yesu. Neno linasema mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Je, hili—je, hili lamaanisha ubatizo, Roho Mtakatifu, au lamaanisha yanipasa kupokea kile kipawa—dhahiri—Yanipasa nipokee tukio dhahiri kwa ubatizo? Nina hamu ku—kujazwa na Roho. Tafadhali niwie radhi kwa maneno mengi kwa vile nimekuwa nikitaka kukuuliza

wewe swali hili kwa muda mrefu. Asante. Na watu wale wameandika jina lao. Ni watu wanaotoka nje ya mji huu.

40 Sasa, hilo ni swali nzuri. Sasa, ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tukio dhahiri ambalo mtu lazima apokee. Sasa hebu na nilifanye wazi hilo kwa muda kidogo. Ona? Sasa, watu wengi wana wa—wazo. . . naamini limepotoshwa. Na labda hapa kwa kanisa na kwa kanisa linalosikiza, huenda kukawa na swali. Sasa, ninapoongea kuhusu kutokuamini kuwa ishara mathubuti ya Roho Mtakatifu ni kunena kwa lugha (si—sikubaliani na hilo) naamini kwa msaada wa Mungu naweza kuthibitisha katika Biblia kuwa hilo ni kosa (ona?), kwa sababu kunena kwa lugha ni kipawa cha Roho Mtakatifu. Wangapi wajua hilo? Uponyaji wa Kiungu ni karama ya Roho Mtakatifu, na hapa Beatles wanafanya hivyo. Ona?

41 Shetani aweza kuiga yo yote ya karama hizo. Wachawi, walozi wanaweza kunena kwa lugha na kuifasiri. Kule nchi za vichakani, wakati mwingi wachawi watanena kwa lugha, wanywe damu kwa fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kufasiri lugha zisizojulikana.

42 Kule katika Arizona wanapokuwa na sherehe za kucheza ngoma ya mahindi, Wahindi hujizungushia hawa nyoka wakubwa wanapojaribu kumsihi Mungu awatumie mvua kwa ajili ya mahindi yao. Wanaiita ngoma ya mahindi. Wanachukua kishada cha mahindi, na kujizungushia, na kufanyiza wingu dogo, nao hucheza ngoma. Kisha mchawi huja akiwa na pembe kichwani mwake, pembe za nyati. Nao hucheza ngoma wamejizungushia hawa nyoka wakubwa, na wachawi na wengi wao wanaovuta kiko na kadhalika, mahali pale. . . Hawawezi kumruhusu mtu mweupe pale wakati huo, lakini nimewatazama kwa darubini, na nina marafiki Wahindi waliohudhuria ngoma zao; hao ni wale ambao si Wakristo, bila shaka. Nao wanacheza hii ngoma ya mahindi huku wameshika nyoka hawa. Na wachawi wanajitokeza, na kujikatakata wenyewe kwa visu, na kadhalika, na mwishowe wanaingia katika roho fulani, na kunena kwa lugha na kuifasiri.

43 Nina—ningewapeleka, umbali usiozidi muda wa masaa kama matatu au manne tokea sasa, mahali ambapo mchawi ataweka penseli mezani, na kuingia katika njozi na mambo mbalimbali, na kupunga mikono yao; na hiyo penseli itainuka na kuandika kwa lugha zisizojulikana, na huyo mchawi angesimama na kuwaambia ninyi inasema nini.

44 Sasa, hiyo si ishara ya Roho Mtakatifu. Ona? Huwezi kutegemea hayo. Huwezi kutegemea tunda la Roho, kwa sababu tunda la kwanza la Roho ni upendo. Na Christian Science hufanyiza upendo mwingi kuliko ye yote nimjuaye, na hata wao wanakana Yesu Kristo kuwa Mungu. Ona? Kuna ishara moja

pekee ya Roho Mtakatifu ninayoijua, na hiyo ni imani halisi katika Neno la wakati huo!

45 Sasa, Wayahudi wale wakaja; walikuwa na dini zaidi kuliko walivyokuwa wale wanafunzi. Walikuwa na watu waliofuzu sana Maandikoni kuliko wanafunzi walivyokuwa, kwa sababu walikuwa wavuvi, watoza ushuru, na kadhalika. Nao walikuwa na imani halisi na imani thabiti katika yale wao walikuwa wakifanya. Sasa, sikiza kwa makini sasa; msilikose! Ona? Inapofikia kuwa matunda ya Roho, kama upendo, nadhani hakukuwa na mojawapo wa makuhani wale ila yule angalimshida Yesu Kristo katika hayo. Yeye alienda hekaluni, akasokota kamba, akawatazama kwa hasira, kazipindua meza zao, na kuwafukuza mle. Sivyo? Biblia ilisema aliwatazama kwa hasira.Ndivyo hasa.

46 Kwa hivyo ona, makuhani hao walikuwa wapole, wanyenyekevu, watu wenye akili. Ilipofikia matunda ya Roho, wangeonyesha matunda mengi zaidi ya Roho kuliko Yesu. Ilipofikia theologia, hawakujua—hamna shule ambayo Yeye alitoka. "Mtu huyu anatoka wapi? Yeye alitoka wapi? Ana kadi gani ya ushirika? Yeye ni wa dhehebu gani? Hatujui yeye anakotoka. Yeye Alikuwa fukara aliyezaliwa kiharamu. Naam, tungemwondolea mbali chini hapa katika dakika chache na kuwaonyesha ninyi kwa torati. . . " Walikuwa na haki kufanya yale waliyofanya ilipofikia hayo. Mbona? Kwa sababu walikosa kuona Yeye alikuwa lile Neno lililoahidiwa la wakati ule. Njia pekee waliyolitambua, Yesu alipotenda Neno kwa kuweza kuwaambia kile walichokuwa nacho moyoni mwao, kile walichokuwa wakitenda. . . Yeye alikuwa Nabii kulingana na Neno la Mungu. Yale Yeye alisema yalitimia, kila Neno, Neno kwa Neno.

47 Yeye alikuwa Nabii wa Mungu, Mtumishi, Mungu Nabii. Si. . . ilikuwa ilikuwa—ilikuwa kabla ya hapo, nabii wa Mungu, na huyu ni Mungu Nabii, si nabii wa Mungu. Hao walikuwa Malaki, Yeremia, na Isaya, na Eliya, na kadhalika, lakini huyu alikuwa Mungu Nabii, si nabii wa Mungu. Mnalifahamu sasa?

Manabii wote walionyesha maisha Yake kwa sehemu, walitimiza fungu lao, lakini katika Yeye mlikuwa Utimilifu wa manabii wote. Hao manabii, lile Neno na Bwana liliwajia, hao manabii, lakini Huyu alikuwa Neno la Nabii, Mtu yule yule. Ona?

48 Sasa, basi, mtu anapompokea Kristo katika hali ambayo Yeye yuko, huwezi kulikubali kama kuwa. . . Ona? Sasa wengine wao husema, "Vema, mimi ni Mlutheri." Vema, hakuna pingamizi kwa hilo, ila Tai hawali hayo. Ona? Hilo lilikuwa mbali kama lilivyokuwa; chakula kipya cha wakati uo huo.

Sasa, watu wale walisema, "Naam, tuna Ibrahimu baba yetu."

Nabii yule alisema, "Mungu aweza kwa mawe haya kumwinulia watoto Ibrahimu." Ona?

"Sisi tu wa *hiki*. Sisi tu wa *kile*."

Hilo halihusiani kamwe . . . Yeye alisema, "Enyi uzao wa nyoka, nani aliyewaonya kutoroka ile ghadhabu? Msianze kusema, 'Tuna Ibrahimu baba yetu' kwa sababu Mungu aweza toka kwa mawe haya kumwinulia watoto Ibrahimu." Ona?

49 Kwa hivyo kuwa mwanatheologia aliyefuzu sana halihusiani nalo. Kuwa mnyenyekevu na mpole halihusiani nalo. Nini kilimfanya Yeye tofauti? Yeye alikuwa Neno lililofanyika mwili, si bile Neno la siku za Musa, Musa alikuwa siku hiyo—Neno; si lile Neno la siku za Nuhu, Nuhu alikuwa Neno kwa siku hiyo; si siku ile—Neno lile la siku za Eliya, Eliya alikuwa Neno la siku hiyo; lakini Yeye alikuwa Neno la wakati uliopo, nao walikuwa wakiishi katika yaliyopita.

50 Jambo lile lile lajirudia! Hiyo ndiyo ishara ya Roho Mtakatifu, Mungu anapokufunulia na unaliona, BWANA ASEMA HIVI na kulikubali. Si vile ulivyo, vile ulivyokuwa, au lo lote lile, ni yale Mungu amekufanyia wewe sasa. Hiyo ndiyo ishara.

51 Yesu alisema . . . Yeye alitupea ishara ya Roho Mtakatifu, Yohana 14. Yeye alisema, "Ninayo mengi ya kuwaambia. Sina wakati wa kuwaambia, lakini Roho Mtakatifu atakapokuja, Yeye atawaambia, atawakumbusha yote niliyowaambia, na mambo yajayo atawapasha habari zake." Hamwoni? Hiyo ndiyo ishara. Huko ni kutabiri na kuwa—kuwa na fasiri ya Kiungu ya Neno lililoandikwa. Sasa, si hiyo ndiyo ishara ya nabii?

52 Mwonaji katika Biblia alikuwa mtu ambaye angetabiri na ingetimilika, kabisa, si eti mtu fulani alimwekea mikono, hicho ni kipawa. Nabii anachaguliwa tangu awali na kuzaliwa nabii. Ona? Maisha yote alikuwa nabii, huo ni huduma. Hapo ndipo watu . . .

53 Mengi ya maswali haya hapa juu ya: "Vema, je, Bibi-arusi ata . . . ?" "Je, *hili* lita- . . . ?" "Kanisa na . . . " Ona? Hu—huwezi kutenganisha yalivyo. Bibi-arusi ni Mteule wa Mungu. Kanisa litapitia . . . Hao ndio wale Hilo linasema, "Yeye atakaye, na aje." Lakini Bibi-arusi ni Mteule wa Mungu.

54 Kuna huduma tano zilizoteuliwa na Mungu. "Kwa kuwa Mungu ametoa Kanisani mitume, manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti." Mungu alifanya hilo. Mwanadamu ana mashemasi na wengineo, na kadhalika, lakini mwaona, bali Mungu aliwaweka Kanisani kwa kusudi la kukamilisha Kanisa—huwezi kuligawanya.

55 Sasa, Roho Mtakatifu, ajapo, ni ushuda kwako (ona?) kuwa Neno hili ni kweli, Neno la siku hizi, si Neno la Luther, Neno, si la Musa. Tunashuhudia ni kweli, lakini ni siku nyingine.

56 Sasa, vipi kama Yesu angekuja na kusema, “Sasa, kama Musa alivyokuja kuwatoa ninyi nyote Misri, nimekuja kuwapelekeni ninyi mahali pengine”? Vipi kama Yeye anasema, “Na tuende tukafanye kazi ya kujenga safina. Mi—mimi ni Bwana Mungu, Ni—nitazamisha ulimwengu sasa. Nitawazamisha walimwengu wote”? Naam, Yeye angekuwa nje ya. . .Ona, Maandiko hayakusema kamwe Yeye angekuja hivyo. ona? Yeye hangelikuwa Masihi. Haijalishi Yeye angejenga safina kubwa vipi, au cho chote angalitenda. Yeye bado si—Yeye hangestahili kuwa Masihi. Haleluya! Naam! Ni ustahilifu! Naam, bwana!

57 I Wakorintho 13 yasema haya: “Ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika.” Kwa hivyo mambo haya yote madogo madogo ya kuruka juu na chini kama mtoto, kujaribu kunena kwa lugha, na mambo haya yote, ijapo ile iliyo kamili. . .Nasi tunayo siku hizi, kwa msaada wa Mungu, ile tafsiri kamilifu ya Neno na thibitisho la Kiungu! Basi ile iliyo kwa sehemu imebatilishwa. “Nilipokuwa mtoto mchanga, nilisema kama mtoto mchanga, nilifahamu kama mtoto mchanga;tokea hapo nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto.” Amina! Naanza kuhubiri na ndipo sitayafikia mambo haya.

282. Ndugu Branham. . .(Je, nilimaliza hilo? Je, nilieleza kuhusu ubatizo wa Roho. . .Naam, hilo lilikuwa juu ya hilo, sivyo, Vema. Kunradhi, kama sitalipata, mnisamehe. Ni. . .Haya ni maswali ya ajabu. Ungekaa usiku kucha kwa swali moja tu, ndugu, na hata usiliguse) **nakudhamini wewe kama mtumishi wa Mungu, kuamini—nami naamini huu Ujumbe wa Kweli. Mke wangu hawezi kunisikiza—asema lo lote—anasema cho chote kuhusu Ujumbe huu, na hatasikiza kanda yo yote. Nina wasiwasi kuhusu kazi yangu pia. Nataka mke wangu aamini pia na kuombea watoto wangu. Ndugu Branham, nataka kuwa rafiki wa Mungu—nataka kupatikana katika mapenzi ya Mungu kuhusu maisha yangu. Nataka kuwa mtumishi Wake.** (Na mtu yule aandika **“geuza.”** Ngoja kidogo) **Nilipokuwa mdogo, nilimwambia kila mtu nilitaka kuwa mhubiri. Sijui yale Mungu anataka nifanye. Niko tayari kufanya cho chote kwa ajili ya Bwana. Wako katika Bwana.**

58 Sasa, swali nzuri. Na mtu huyu ni myofu wa moyo. Mke wake, mwenziwe aliye sehemu yake. . .Niongeze kitu fulani hapa kwa hilo? Ndugu zangu, nasema hili katika Jina la Bwana. Hivi karibuni, Bwana akipenda, nafikiri nitafanya kanda hiyo juu ya *Ndoa na Talaka* (ona?), niilete papa hapa maskanini. Kama itatenganisha, itabidi itenganishe. Lakini tutayathibitisha kuwa ni Neno la Bwana.

59 Tazama, ndugu zangu. Sikizeni hili. Je, mwajua mara nyingi unapata mwenzio asiyekufaa hapa duniani? Kisura fulani aliye na macho ya hudhurungi, au samawati, au

kijivu anakuvutia akakuingiza katika janga ambalo—ambalo haikukupasa kumsikiza. Wanaume wengi wanatambua hilo.

60 Mwanamume anayetaka kuoa yampasa kwanza aliendee kwa maombi. Hampaswi kuchagua wanawake kwa kuwa warembo upande wa nje, lakini warembo upande wa ndani, mtu atakayekuwa mama kwa watoto wako.

61 Najua hili litasikika baya sana kwa mhudumu kusema hili mimbarani. Lakini nilikuwa nikienda na—na wanunuzi wa ng'ombe za kufuga Magharibi, nao wangetaka kuanzisha kundi. Nami nilijifunza chungu nzima pale ambayo—nilipowaona hao madalali na mambo waliyokuwa wakifanya, hao wanunuzi. Nilikuwa nikiambatana na mzee mmoja, alihudhuria kanisa hili pamoja nami, nami nilimleta kwa Kristo, kafiri halisi hapo kwanza, Bw. Jeverez. Wengi wenu mnamkumbuka, mfugaji wa kule Colorado. Tungeenda, nao wangefikia—ng'ombe.

Nilimwona ndama mdogo wa kufugwa siku moja anauzwa dola elfu kumi na moja, ndama mdogo; alikuwa bado hajapata mimba. Nami nilisema—na Jev alisema, "Kama ningekuwa na pesa hizo, ningemnunua ndama huyo."

Nami niliwaza, "Sasa, yeye ni mfugaji; yeye aifahamu kazi yake." Nilimwuliza, "Jev, mbona wewe u . . . Ustahili wake ni nini? Yeye ni wa aina ya Hereford. Huyo aliyenunuliwa kitambo kidogo kilichopita kwa dola mia tatu, kwangu, alionekana kama ndama mkubwa zaidi na kadhalika."

62 Yeye alisema, "Tazama, Billy, kuna jambo moja ambalo haufahamu katika ununuzi wa ng'ombe." Kasema, "Nadhani yapasa ushikilie kazi yako ya kuhubiri." Lakini kasema, "Haufahamu ng'ombe." Yeye akasema, "Sasa, mtazame ng'ombe yule chini pale." Tukaenda kule chini. Kasema, "Waona huo mkodoo jeuri wa macho yake?"

Nilisema, "Naam."

Kasema, "Watoto wake, na wajukuu wake, na wajukuu wa wajukuu wake bado watakuwa na huo mkodoo jeuri." Na kasema, "Watajiharibu kwa kuzurura. Hatawahi kamwe kuwa mama kwa ndama zao." Kisha kasema, "Hungeweza kamwe kuwanonesha; hawatakuwa kamwe na nyama nzuri." Akasema, "Tazama huyu ndama mdogo hapa anayeuzwa. Mtazame jinsi anavyoonekana mpole. Tazama huo mtazamo mtulivu usoni wake, huo mtazamo mwema, hakodoi macho." Kasema, "Yeye atakuwa mama halisi kwa ndama zake; na ndama za ndama zake, na ndama za ndama zake wataendelea kuwa vivyo hivyo." Kisha kasema, "Hao wote watakuwa mama, wakipata aina nzuri ya ndume wa kumzalisha ndama huyo (ona?), hilo litafanya watoto wao. Lakini huo mtazamo wa kukodoa macho usoni mwao kila mara utazaa kundi baya la ng'ombe, kama mtu anajaribu kununua ng'ombe."

Nilisema, "Naam, bwana! Asante."

63 Na jambo lile lile lahusu wanawake. Mchukue yule aliyejipaka rangi usoni na kukodoa macho, anaonekana kama mnyama fulani, kujaribu kujigeuza mwenyewe toka kwa mwanadamu, yeye hataweza kamwe kufanya cho chote. Atakimbia daima. Na Ukristo si urembo wa nje, ni wa ndani; wa amani, utulivu, kujipamba katika roho wa amani na utulivu, ambao ni thamani kuu mbele ya Bwana. Hilo ndilo tunalotaka kutazama kwa wanawake, na kwa wanaume, na kwa ye yote yule. Sasa . . .

283. Ndugu Branham: Maswali: Je, mwanamke Mkristo aweza kuvaa vito rahisi kama mikufu au lulu?

64 Vema, Dada najua hili ni muhimu sana na lamaanisha mengi kwako, na lamaanisha mengi kwangu wakati wewe unapotumainia ya kwamba ningekwambia kweli. Sasa kumbuka, Biblia ilisema, "Mnapojipamba, msijipambe kwa—kwa vito vya gharama kuu, na lulu, na namna zote za kujipamba kwa vito, lakini na kuwe kujipamba kwa roho ya amani, na utulivu, na upole (ambalo nilinukuu hivi punde tu) ambako ni kwa thamani kuu mbele za Bwana.

65 Sasa, sikusudii kwa hilo, Dada, kwamba kama ulikuwa na pini . . . Sasa, hili ni mimi si Bwana. Kama ulikuwa na pini uliyotaka kujipambia, au mkufu mdogo ambao mume wako alikupa, au labda—kitu fulani kama hicho ulichojipambia, sasa, kwangu, sidhani hilo ni baya. Sasa, huyo ni mimi. Sasa kumbuka, najifanya mwenyewe dhahiri; hayo ni maoni yangu. Lakini nafikiri ni jinsi unavyoliendea; ni jinsi unavyolifanya. Ona? Ni kusudi la kufanya hivyo. Na unapoliona likikukwaza, basi liachilie. Lakini nadhani kama ulivaa pete yako ya arusi . . .

66 Sasa, najua ninyi watu wa Nazarini, ilikuwa kwamba hata hamngebatiza mwanamke aliyevalia pete ya arusi. Ona? Si—siamini kuwa hilo linafaa. Katika Biblia walivaa pete za arusi, ila tu waiita ubamba, kuzunguka kichwa chao, vipande tisa vya sarafu ndani yake. Lakini nina—kuonyesha kuwa wameolewa. Sasa, nadhani hilo ni sawa.

67 Kama wanawake wanataka kuvaa na—na kujifanya wenyewe waonekane wazuri, wasafi, wa kimama, naam, nadhani hakuna ubaya hapo, kwangu. Lakini unapoanza kuweka kitu kile ndani yake kujionyesha kidogo, basi umekosea. Ni nia yako.

68 Je, ninyi wanawake mnakumbuka hapa si muda mrefu uliopita walikuwa na kile walichoita "rinda kashifu"? Nafikiri zinarudi tena, au zina—zinadhaniwa kuwa . . . Sasa hazikashifu badala ya kukashifu. Lakini walikuwa na mchezo si muda mrefu uliopita . . . Walikuwa na wasichana, vijana wanawake . . . Na bila shaka, wazee pia wangelifanya pia, kwa sababu wana—wote wanataka kuwa vijana. Sikusudii ninyi akina dada, nakusudia

wanawake wa ulimwenguni. Nao wangekata rinda zao—zao kuzifupisha sana, karibu futi moja juu kila wakati, ndipo wavae baadhi ya nguo za ndani waonekane warembo. Na wakati walipopiga hatua, ingeonyesha hizi nguo za ndani na zenye kimia, au pindo, au cho chote kilichokuwa juu yake. Ambavyo, mwajua . . .

69 Kulikuwa na m—msichana aliyekuja kwangu, aliyekuwa msichana M-Dunkard, alikuwa tu amepokea Roho Mtakatifu hivi punde. Yeye alikuwa wa Assemblies of God, na hiyo ilikuwa katika Fort Wayne, Indiana, ambako nilioa. Naye alinijia, bibi mdogo, na mzuri, naye alisema, "Ndugu Branham, nataka kukuuliza swali."

Nilisema, "Vema, Dada kuna nini?"

Yeye alisema, "Je, wadhani ni kosa kwa msichana ku—msichana Mkristo kuvaa 'rinda kashifu'?"

Nilisema, "Dada, hili ni jambo moja amba—ambalo sifahamu. Nini 'rinda kashifu'?" Naye aliniambia ilikuwa nini. Nili . . .

Yeye alisema, "Linaonyesha rinda ya ndani."

70 Nilisema, "Nini—nini kilicho ndani ya mwanamke ambacho kinamfanya atake kumwonyesha mwanamume nguo zake za ndani? Nini kinge- . . . Msichana Mkristo ana shughuli gani—gani kufanya kitu kama hicho? Je, ungewazia Mkristo?"

71 Sasa, tazama, mwanamume, hakuna mengi kwake inapofikia kwa mwili. Na yeye, kama angeenda nusu uchi, inge—hakungekuwa na kashifa yo yote kwalo. Si kuwaunga mkono wanaume, lakini wao . . . Mwajua hilo—ni mwanamke wa namna gani angejaribiwa na mwanamume aliyevua shati lake na amevalia suruali fupi au cho chote alichovalia? Anaonekana kitu kikubwa kizee kisicho na maumbo ya kupendeza, anaonekana kitu ovyo na cha kutapisha, kitu cha—cha kuchukiza. Ona wanaume hawa nje hapa . . . Vema, nafikiri ingemfanya mwanamke atapike kutazama kitu kama hicho. Kama yeye alikuwa na . . . Lakini sasa, mchukue mwanamke na mweke hivyo, hilo ni hekalu tofauti. Mwafahamu? Vema.

72 Lakini nadhani kuhusu mkufu, au . . . Sasa, ukienda ukijijaza hivyo kama kwamba ulipitia katika duka la kujichagulia bidhaa hapa chini ukiwa na sumaku, na—nafikiri kuwa . . . Kuradhi hilo, sikukusudia kusema hilo hivyo, lakini hilo—hilo ni kosa.

73 Kama lo lote lilinifanya nipinge mara ya kwanza—lilinifanya niaibike juu ya Amerika, lilikuwa . . . Nilikuwa Switzerland siku moja, na Ndugu Arganbright tulipata mahali pazuri kule karibu na Lausanne ambapo tungepata mnofu mkubwa, mwororo, karibu ukumbwa huu, wenye uzito wa karibu robo tatu ratili, nadhani, kwa karibu senti thelathini katika pesa za Amerika. Ee, tuliishi kama wafalme! Kila siku tungeenda chini kule. Na

wao wote kule hunywa divai, mwajua; maji yao si mazuri. Nami singekunywa divai hiyo, kwa hivyo nilijinunulia kopo ndogo toka kwa—kwa duka la madawa lilikuwa na maji yaliyosafishwa. Nami nilibeba kopo hilo ko kote nilikoenda. Nadhani kila mtu alidhani, "Kijana yule anajibebea divai maalum." Kwa hivyo nililibeba mkononi mwangu. Tulienda chini kule hadi mahali ambapo—waiuza hii minofu, na siku moja *Bi. Amerika* akawasili: Aliendesha Chevy muundo 28, alikuwa na mbwa mwenye manyoya mengi ameketi pajani mwake na akaja naye ndani mle, naye alikuwa na . . . Hao wanawake wawili walikuwa na ghala nzima ya vito, vito vikubwa mno na virefu, na pete za masikio, zikining'inia, na rangi; na wote wawili wana umri wa miaka hamsini, wazee kama mimi. Na ungedhani walitaka kuwa na miaka kumi na mitano. Lakini wanajaribu kufanya nini? Wanajaribu kuendesha kwenye barabara ya maishani wakitazamia kioo cha kutazamia nyuma, wakitazama nyuma kwa yale waliyokuwa.

74 Sasa, Wakristo hawafanyi hivyo. Mkristo hajaribu kuwa kile alichokuwa; yeye hatazami alikokuwa, anatazama anakoenda. Ona, ona? Usivutiwe na vile ulivyokuwa wakati huo; umemaliza maisha hayo. Haturudi kamwe kwa hayo; hayo ni katika yaliyopita. Na mtu ye yote anayejaribu kuendesha kwenye barabara ya maishani akitazamia kwa kioo cha kutazamia nyuma ataangamia, na hata nanyi pia kwa hii barabara ya Kikristo. Usitazame nyuma jinsi mlivyokuwa, tazama kile utakachokuwa. Paulo alisema, "Nikisahau yaliyopita, nakaza mwendo niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu."

75 Sasa, lakini ilikufanya uone haya. Walileta huyu mbwa mdogo anayenuka ndani mle na kumweka juu ya meza! Sasa, hilo lingemfanya ye yote atapike! Na kucheza-cheza na mbwa yule papo hapo, wakimketisha juu pale kwa mikono yao, halafu waende wakale kwa mikono iyo hiyo! Kisha mtumishi wa hotelini akaja pale, na kupayuka-payuka maneno fulani. Dk. Guggenbuhl alikuwa pamoja nami; yeye alianza kucheka, akiangalia upande.

Niliuliza, "Nini—alisema nini?"

Kasema, "Mtumishi yule alisema, 'Ondoa hicho!'"

Wao walisema, "La, yeye ni Mwamerika; achana naye." Yaani, "Yeye hajui bora kuliko hayo." Ona?

76 Nilipoenda Saint Angelo kule Rumi (sasa, waza hili), kule Vatikani katika Rumi, Italia, walikuwa wameweka ubao kule Saint Angelo: "Kwa wanawake Waamerika; kabla hamjaingia pango hili la kuzikia watu, tafadhalini vaeni nguo mpate kuheshimu wafu"—kanisa Katoliki. Ona?

284. Swali: **Ndugu Branham, Bibi-arusi atakuwa wapi dunia itakapolipuka na kuteketezwa? Itakuwa mahali fulani kama vile wana wa Israeli walivyokuwa Gosheni**

mapigo yalipoanza? Je, Bibi-arusi atakuwa duniani haya yatakapotukia? Kama ndivyo, wapi? Je, Bibi-arusi atakuwa mahali pamoja wakati wa wunyakuliwa?

77 Bibi-arusi, dunia itakapolipuka . . . Wakati wa kunyakuliwa utakuwa kufufuliwa kwa wafu na kukusanyika kwa walio hai, kwa ajili—pamoja na walio hai, kusudi kunyakuliwa kutendeke. Sasa, lakini Bibi-arusi . . . Sasa, Ona, moja ni kunyakuliwa nyuma huku kabla ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Na dunia itakapoteketea ni nyuma hapa baada ya Ule Utawala wa Miaka Elfu na baada ya ile hukumu ya kile Kiti Cheupe cha Enzi. Ona? Watakatifu watakuwa wamepiga kampi kwenye mapana ya dunia Shetani atakapokuja kuuzingira ule Mji unaopendwa kisha Mungu atanyesha moto na viberiti toka Mbinguni na kuwaangamiza. Vema. Naam, hiyo ni Maandiko.

285. Pia Ndugu Branham, naamini mwanamke apaswa kumtii mumewe. Lakini kama mwanamke Mkristo ana mume mwenye dhambi ambaye hata mojawapo wa ibada zako—hahudhurii mojawapo wa ibada zako na ha—na ataka mke wake awe akifanya vitu, kukata nywele zake, kuvaa suruali fupi, na kuenda mahali pabaya, je mwanamke huyu apaswa kumtii mwanamume huyu hivi? Tafadhali eleza hili dhahiri mno, kwa kuwa hili ni swali ambalo huulizwa mara kwa mara.

78 La, Dada, haupaswi kumtii mtu kama huyo. La, hasha. Kwa sababu hiyo utaacha kila kitu na umtegemee Mungu. Sasa, jambo ni . . . Ukitaka—mwanamume yule akitaka kuishi nawe, na wewe u—dumu Mkristo . . . Lakini kama yeye atakufanya uvae suruali fupi, ukate nywele zako, na kufanya mambo haya mengine, na mahali pabaya, basi utafute kwanza Ufalme wa Mungu na haki Zake. Haikupasi kufungwa nira na mtu kama huyo. "Lakini mradi tu," Biblia inasema, "kama mwanamke huyo anataka na mwanamume anataka wakae pamoja (mnakumbuka hayo), basi . . . "

Na sasa, haya, sikuandika hilo Andiko, kwa sababu niliyachukua tu (mwaona?) dakika chache zilizopita. Nachukua moja sasa na ndipo sina wakati . . .

79 Lakini Paulo alisema mradi tu wao—mwanamume asiyeamini akiwa na asiyeamini—au mwanamke anayeamini au kadhalika, na mke anayeamini abaki na mume anayeamini, mradi tu si kinyume sasa cha Mungu. Kama yeye anapenda kukaa naye . . . "Endelea, mpenzi, ukitaka kwenda kanisani ni sawa; lakini mimi siendi. Siamini hilo; sina uhusiano wo wote nalo. Lakini wewe endelea; hilo ni sawa." Lakini mume yule asemapo, "Huwezi kufanya hivyo." Sasa hilo ni jambo tofauti, Wewe hufungwi kwa hilo basi; unatenga kila kitu kwa ajili ya Mungu.

286. Ndugu Branham, je, (hebu tuone.)**...mtu ambaye—ambaye alimtaliki mkewe ambaye yungali hai kisha akaoa tena kabla hajakuja kwa Ujumbe anaweza kuhudumu?**

80 Vema, katika I Timotheo 3:2, ukitaka kuandika hayo, na Tito 1 hadi 6 (niliandika hayo), ninataka msome hayo kwa swali hili. Ona? Kama mtu—kama mtu akitaka kazi ya askofu au mhubiri (kitu cho chote kanisani), imempasa awe na mke mmoja tu. Naam! Mhudumu. Sasa, hayo ni I Timotheo 3:2, na Tito 1 hadi 6. Sasa, Tito 1 hadi 6, naam! Vema. Sasa, tazama kuwa Biblia ilisema kwamba huyo mtu ambaye ni mhudumu katika nyumba ya Mungu atakuwa na mke mmoja. Basi.

287. Mpendwa Ndugu Branham, yapata miaka kumi iliyopita Mungu alinijia basi na kuponya karama ya upendo—au akanifunulia karama ya upendo ni nini, na vivyo hivyo ombi langu ni kwa—ya kwamba nitarudi. Nitaipokea kabla sijafa? Je, mume wangu atasikia Neno, na inanipasa nifanyeje?

81 Hilo ni swali kabisa. Sasa, yeye alisema...Sasa, mambo yalivyo hapa, au—akisema "Mume wangu," kwa hivyo nadhani haina budi kuwa ni mwanamke aliyesema hili. Sasa, yeye alipoteza upendo wake wa kwanza. Ona? Yeye—yeye alipoa katika Roho. Sasa, Dada, labda kwa sababu wewe bado huja kanisani na kufanya yaliyo mema, haujapoteza wokovu wako, lakini umepoteza furaha ya wokovu wako. Daudi alimlilia Bwana wakati mmoja, "Bwana, unirudishie furaha ya wokovu wangu." Wewe bado u Mkristo, lakini nina—kile unachotaka kufanya, Dada, ni kuachilia kila kitu ujuacho, na kumtafuta Mungu, na kuomba.

82 "Je, mume wangu atasikia Neno, na nifanyeje?" Kama nilivyosema asubuhi hii, kolea chumvi: "Ninyi ni chumvi ya dunia." Mume wako atatazama maisha yako masafi, na mume ambaye si mwamini atatakaswa kwa Bwana na mke wake anayeamini. Mtafute Bwana, dumu ukiwa mpole, na kuomba kila wakati, ukimpa Mungu utukufu, na ukiwa mwema kwa mumeo kwa mradi tu yeye anataka kuishi pamoja nawe hivyo.

288. Kwa ibada za Jumapili: Mwanamke akitenda tendo baya na...(Sasa, ngoja kidogo;heri nijisomee hili kwanza. Mwaona? [Ndugu Branham ajisomea swali—Mh.] Vema. Hili ni sawa.) **Mwanamke akitenda tendo baya na m—mwanamume aliyeoa, atubu na alirekebishe na mumewe kulingana na Maandiko, je, yeye anapaswa kwenda kwa yule mke wa mwanamume aliyehusika, hata kama mke huyu hajui lo lote juu yake; au ni wajibu wa mwanamume yule kumwambia mkewe kwanza; au je, inapasa aumizwe kwa vyo vyote vile? Tunaweza kwenda umbali gani na huku kuomba msamaha wakati mambo hayo yamekwisha kabisa, na wakati urafiki unahusika?**

83 Vema, Dada yangu mpendwa, kuna jambo moja pekee ambalo umefanya ambalo ni sahihi. Ulihusika, nadhani, au mtu fulani unayemjua alihusika, katika tendo baya, kwamba ulimchukua mume wa mwanamke mwingine na kujuana naye kimwili. Na ulipofanya hivyo, pale ulianguka toka kwa neema yako. Kisha ukatubu, na hungetubu hadi urudi kwa mwanamume huyu na kulisahihisha. Yakupasa umchukue mume wako na umwendee huyo mwanamume, ambalo ulifanya. Na hilo ndilo jambo lililokupasa kufanya; hilo ni Maandiko—ilikupasa kufanya.

84 Mwanamke fulani alinijia si muda mrefu uliopita toka papa hapa Louisville, ya kwamba . . . Yeye ni kijana mwanamke. Alienda na mwanamume fulani ki—kisha yeye . . . Yeye alijua alikuwa akifanya kosa. Naye akaondoka mjini, na akaenda katika mji mwingine mbali sana, na kugeuza jina lake, akaishi na watu fulani. Na mwanamume huyu alimfuata na kumwambia mwanamke huyu alipofika kule, yeye angemtoza hongo. Sharti aendelee kuwa mchumba wake haramu, la sivyo, atamkashifu. (Na mwanamke yule alipokuwa kule, akaolewa na Mkristo mzuri.) Naye akasema kama hangeishi naye, yeye angefichua jambo hilo lote—akamtisha; kwa hivyo, yeye akalazimika kuishi na wanaume wote wawili, ambayo ilikuwa kosa, badala ya kuonyesha msimamo wake mwanzoni. Kisha akapata mtoto, na sasa, huyo msichana ana umri wa miaka kumi na minane na hajui nani hasa ni baba yake halisi. Sasa, mwanamke huyu akafikia ugumba wake, na sasa anajuta. Sasa, yeye afanyeje? Nilisema, "Kuna jambo moja pekee . . . "

Yeye alisema, "Nikimwambia mume wangu, yeye atanitaliki; na kama mimi—binti yangu akijua, "yeye atajiva."

85 Nami nilisema, "Ukiliweka moyoni mwako, utaenda kuzimuni. Naam, chagua likufaalo." Kuna jambo moja tu la kufanya, ni kuanza upya. Ndivyo hasa. Kuwa mwaminifu.

86 Mnajua, wakati mwingi katika maono, jinsi watu huja, wanaume kwa wanawake; Roho Mtakatifu anayachambua mambo ambayo wamefanya kote maishani na (mmesikia kuhusu hayo na kuyaona, mnajua. Ona?)—na kuwaambia wao mambo yanayowapasa kufanya.

Wao husema, "Vema, nime—nimekwisha kuyarikebisha kwa Bwana." Lakini yakupasa kumwambia mume wako au mke wako. Naam. Yakupasa kukiri hilo.

87 Sasa, mtu huyu, kama mwanamke huyu ndiye ana hatia, yeye amelitekeleza; yeye alienda kwa mume wake. Sasa, wewe umejiondoa lawamani, Dada, kwa sababu kati . . . Uli—ulizini dhidi ya mume wako. Ulienda kwa mume wako na kujiondoa lawamani kwa mume wako, halafu ukaenda kwa mwanamume yule na mumeo na kujiondolea lawama kule. Huna lawama. Kama mume wako anaendelea ku—kutaka kuishi nawe, hilo

ni juu yake. Si lazima afanye hivyo sasa, lakini aki—lakini kama akitaka kuishi nawe na anakusamehe, basi wewe uwe bibi kutosha na usithubutu kamwe kuwa na hatia ya tendo kama hilo tena. Lakini yeye asipokusamehe, ndipo hiyo—hiyo ni juu yake. Yeye aweza kukutaliki. Sawa hasa.

88 Lakini sasa, mwanamume uliyezini naye, sasa, yeye ndiye apaswa kwenda kwa mke wake amchukue mke wake na aje tena kwako. Umetekeleza sehemu yako, sasa ni wakati wake kutekeleza sehemu yake. Ona? Kundi la pili . . .

89 Mwanamke huyu alizini na huyo mwanamume, naye akamchukua mumewe, akaungama, na akaenda kwa mwanamume yule akaungama, na kulirekebisha. Sasa, yule mwanamume wa pili alikuwa mwanamume alieoa pia; sasa, mwanamume yule apaswa kwenda kwa mkewe na amchukue mkewe na arudi kwa mwanamke huyu. Ndipo ni sawa. Mwafahamu ninalomaanisha? Limetatuliwa wakati huo. Lakini nje ya hayo, bado utakuwa na hatia, na moyoni mwako utahukumiwa.

90 Nilikuwa na mwanamke si muda mrefu uliopita juu pale aliyekuwa na hilo tangu vita vya Kwanza vya Dunia. Naye alisema, "Ee, Ndugu Branham." Yeye alikuwa ametumia mamia ya Dolla kwa daktari wa mawazo na kila kitu. Nilikuwa nimeketi pale nikimtazama yeye chumbani humo. Meda alimleta juu pale. Yeye alikuwa ameketi pale akiviringisha kitambaa mkononi mwake hivyo, kasema, "Naona kama ulimwengu utalipuka, na mimi." yote hivyo.

Nilizidi tu kuketi pale. Nikasema, "Sasa, kuna kitu fulani kuhusu . . . Una kitu fulani maishani mwako mahali fulani?"

"La, mimi ni mwalimu wa shule ya Jumapili."

Nilisema, "Vema." Niliketi pale kidogo na kutazama. Nikasema, "Naona motokaa ndogo ya kijani, nawe uko pamajo na mwanamume mwenye nywele za shaba, na gari la moshi karibu ligonge motokaa ile."

. . .?. . . Yeye kasema, "Usimwambie ye yote hilo!"

Nilisema, "Mume wako alikuwa jeshini wakati huo."

Yeye akaanza kulia, akaruka juu, "Usimwambie ye yote hilo." Ona? Hayo yalikuwa chini kule katika dhamiri yake. Yeye kasema, "Nimeungama hilo kwa Mungu zamani sana."

91 Nilisema, "Lakini ngoja kidogo. Hukumtendea Mungu kosa. Ulitenda kosa dhidi ya nadhiri yako ya ndoa. Yakupasa urudi kwa mumeo na ulirekebishe kwanza."

Yeye alisema, "Yeye ataniacha."

Nilisema "Mungu amekuacha haidhuru. Kwa hivyo, nani unayetaka akuache?" Nilisema, "Mwendee."

Naye alisema, "Ee, ni—ni. . .Yeye atafanya *hili*, nami nina watoto wawili."

Nilisema, "Vema, hayo ndiyo yote ninayoweza kukwambia. Madaktari wa mawazo hawakuvuta hayo kwako, lakini Roho Mtakatifu ameyafunua; na sijawahi kamwe kukuona wewe maishani mwangu."

Yeye alisema, "Hilo ni kweli hasa!" Kasema, "Vema, si—siwezi kumwambia."

Nikasema, "Vema, ni. . .nina furaha nilikutana nawe." Nikaingia katika chumba kingine, naye alirudi tena ndani mle.

Meda alisema, "Yeye anakutaka ndani mle tena."

Nilienda mle; nami nilisema, "Unataka nini?"

Naye alisema, "Ndugu Branham, siwezi kumwambia hayo mume wangu!"

Nilisema, "Mume wako ni mtu mwenye nywele nyeusi."

"Naam!"

Nilisema, "Yeye ana kitu kile kile kukiungama kwako."

Yeye alisema, "Lo, si mume wangu!"

Nilisema, "Afadhali uende kamlete na mje hapa." Nilisema, "Je, unamjua mwanamke *fulani*, anayevalia nguo nyekundu—nyeupe, anayefanya kazi katika afisi ya kampuni ya mitokaa aina *fulani*?

Yeye akasema, "Bila shaka!"

Nikasema, "Si wanamwita jina *fulani*?"

"Naam!"

Nilisema, "Majuma mawili yaliyopita wao waliketi chini ya mti Ulaya wakiwa na wakiketi katika motokaa ndogo ya Chevrolet yenye rangi ya hudhurungi yenye leseni nambari *fulani na fulani*, na walikuwa katika tendo lilo hilo."

Yeye alisema, "Si mume wangu!"

Nilisema, "Vema, nenda kamlete na mje hapa."

Yeye aliondoka. Dakika chache, hawa hapa. Yule mwanamume kasema, "Ni kweli!"

Nilisema—nilisema, "Mwaona? Sasa nendeni mkamwambie Mungu!"

92 Lakini kwanza, unapokuja madhabahuni na kukumbuka kuna jambo fulani, nenda kwanza ukasuluhishe hilo. Na mradi tu yule mtu mwingine hapa ana hatia ya kutokumwambia mke wake. . .Mwanamke huyu amerekebisha yake. Sasa, ni juu yake na mume wake. Lakini mwanamume huyu mwingine na mkewe yawapasa warekebishe hilo. Na huwezi. . .Haijalishi utafanya nini, litakusumbua mradi tu ungali hai mpaka utakapoliungama lote. Kuna njia moja pekee ya kulifanya: Liungame. Hata kama

litakuchuna ngozi, fanya hivyo haidhuru. Sema ukweli, ndipo umefanya haki. Amina!

93 Naweza kusikia wengi kwenye kanda wakisema, "Sivyo." Lakini jaribu tu hivyo wakati mmoja na uone kama sivyo. Vema.

289. Swali la Jumapili asubuhi: (Nasikitika ni wakati huu, lakini . . .) **Mara tu mtu ampokeapo Roho Mtakatifu, au ubatizo wa Roho Mtakatifu, je, kuna tofauti? Je, mtu hunena kwa lugha? Kama si kila mara, ni dhihirisho gani hujulikana?**

94 Vema, waweza kuwazia mama akimzaa mtoto na asijue? Ingalimpasa awe amezirai kutojua. Wala nawe huwezi kupokea Roho Mtakatifu na usijue. Kuna kitu fulani kitendekacho ndani yako. Ona? Kuna kitu fulani kinachokubadili. Mwongozo wako wote, mwongozo wako wote wa kiroho unafanywa upya tena, na unakuwa kiumbe kipya katika Kristo, kama Biblia isemavyo, *kiumbe kipya* katika Kristo. Unajua.

95 Sasa, unasema, "Ndugu Branham, basi huamini kuwa mtu apaswa kunena kwa lugha kumpokea Roho Mtakatifu." Si kwa kuthibitisha yeye ana Roho Mtakatifu.

96 Ningependa kama kila mshiriki wa kanisa langu angenena kwa lugha. Ningependa hao wafanye hivyo, na kama—naamini kama ukimwomba Mungu, Mungu atakupea. Lakini hebu niwaambieni; najua watu wengi wanaonena kwa lugha na hawana Roho Mtakatifu. Na hakuna mhudumu aliye mwaminifu kwa kusanyiko lake ila yule ataliambia kusanyiko lake vivyo hivyo. Shetani aweza kuiga hilo.

97 Paulo alisema, "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, nikijitoa mwili wangu niungue moto kama sadaka, nijapofahamu siri zote za Neno, nijapotoa mali zangu zote kwa maskini, na mambo haya yote, na sina upendo, ningali si kitu. Nina imani kiasi cha kuweza kuhamisha milima na mengineyo; ningali si kitu." Ndipo yeye alisema, "Iliyo kwa sehemu itabatilika, ijapo ile iliyo kamili," au ile iliyo kamili *itakapojulikana*.

Sasa, nina swali juu ya hilo. Natumai nitalifikia usiku huu, kuhusu nini kilitendeka zile Muhuri zilipofunguliwa. Nami nadhani labda utaelewa swali hili moja kwa moja.

290. Swali: **Ndugu Branham, tufanyeje? Kitu fulani kimekaa juu yangu ambacho siwezi kukishinda. Majira ya mwisho wa mwaka uliopita niliota nilipotelea katika mchanga mweupe wa bahari. Kulikuwa kunakuwa giza; singepata njia. Ndoto hii imekuwa nami tangu mwisho wa mwaka uliopita. Sasa, niko kama mtu anayepapasa gizani. Mwanangu (E-r-v-), Ervin, na mke walihusika katika ndoto yangu. Sasa, wao nao pia wamo gizani. Tuko kwa hali ya kukata tamaa—tumekata tamaa. Naamini Mungu atakuonyesha wewe ni nini—yale yaliyo mioyoni mwetu**

sasa. (Bi. . . .Ee, vema.) **Kama tumekosea au kutenda dhambi mahali fulani, twambie. Tunataka kuwa sahihi.**

98 Simjui mwanamke huyu, lakini najisikia tu kama uko hapa, bibi, kwamba shida yako ndiyo hii. Umeacha kitu fulani kitendeke kwako ambacho kimekufanya ujawe na fadhaa, kwa sababu kuwa katika "mchanga mweupe wa bahari" yamaanisha usafi na haki. Na unamruhusu Shetani akusumbue. Ndoto yako ilionyesha kuwa hakuna cho chote kibaya. Wewe umeshikwa tu na fadhaa, na kwa kufanya hili na kuwaza hili, unafanya jamaa yako yote ishikwe na fadhaa. Acha kufanya hivyo; dai haki zako ulizopewa na Mungu. Ndoto yako yathibitisha kwa kufasiriwa ya kwamba wewe uko *katika* mchanga mweupe wa bahari. Kila kitu ni sawa. Ni wewe, mwenyewe, uliyeshikwa na fadhaa.

99 Na unapomfanya mmoja wa jamaa ashikwe na fadhaa, inaingilia anayefuata, kisha anayefuata, na muda si muda ninyi nyote mnagombana na kuendelea. Na mmoja wa jamaa akiudhika na jambo fulani, linamuudhi mwingine, na mwingine, na mwingine, muda si muda jamaa yote imeudhika. Ni Shetani. Ndipo mmoja wa jamaa akifurahi, na wengine wafurahi pamoja naye. Kwa hivyo kila mmoja wa jamaa ajaribu kufanya hilo.

100 Jaribuni, kila mmoja wenu enyi watoto, kusaidia baba zenu, na mama. Enyi akina mama, ninyi. . .Baba, jaribuni kuwasaidia watoto. Msiruhusu huyo roho wa huzuni, asiyeamini awazingire. Ninyi ni Wakristo. Mmezaliwa kwa Roho wa Mungu. Ninyi ni chumvi ya dunia. Mna haki mliopewa na Mungu. Na Biblia ilisema, "Yakiwepo yo yote yenye sifa, ukiwapo wema wo wote, yatafakarini hayo." Msiwaze kuhusu jambo baya.

Na Dada, nadhani hiyo ndiyo shida yako, Dada mpendwa.

Ningekaa kwa hilo wakati mrefu, lakini kulingana na yale niliahidi, dakika ishirini tu. . .Na ningetaka kufikia mengi ya haya. . .kama sivyo, yarudishe kwenye dawati nami nitayapata tena.

291. Wengine husema Ndugu Branham ndiye yule Mwana wa Adamu. Nilidhani ni ile Nguzo ya Moto ndiyo iliyokuwa yule Mwana wa Adamu. Je, nimekosea?

101 Vema, hilo ni swali nzuri, nzuri sana. Lakini mimi si yule Mwana wa Adamu, bali ni mwana fulani wa adamu. Kuna tofauti kubwa. Yesu Kristo alikuwa yule Mwana wa Adamu, yule Mwana wa Mungu, yule Mwana wa Adamu, yule Mwana wa Daudi.

102 Sasa, sababu ambayo swali hilo labda liliulizwa na mtu huyu au limesemwa, ni sababu watu hunichukua mimi kama mtabiri, ambalo sijawahi kamwe. . .Nina swali lililoulizwa ndani humu linalonishambulia mimi kwa hayo. Ona? Lakini ni—ni—ni—ninyi—ninyi. . .Ninaposoma maswali haya mtaona sababu gani ninajibu mambo jinsi nifanyavyo. Hata nitakapoongozwa

dhahiri kufanya jambo fulani (ona?), ndipo nita—nitakaposema lile napaswa kusema. Lakini wakati huo haujafika.

103 Kwa hivyo mimi si yule—yule Mwana wa Adamu mtiwa mafuta. Sidai kuwa nabii Wake. Wakati mwingi nimesema bila kujua nilisema, kajisikia mwenyewe katika kanda. Lakini nasema hilo wakati mwingine, kwa sababu ukitaka kueleza maana yake, nabii katika msemo wa Wiingereza, ni "mhubiri" tu. Mtu ye yote ajua hilo; chukua kamusi. Ona? Nabii ni "mhubiri" katika kamusi ya Kiingereza. Lakini katika Kiebrania au Kiyunani, *nabii* ni "mtabiri, mtu aonaye mambo kabla hayajatukia na kutabiri mambo." Lakini chini ya tafsiri ya Kiingereza, *nabii* ni mtabiri.

104 Kwa hivyo sitaki kujiita mwenyewe lo lote ila ndugu yenu. Mimi ni ndugu yenu, na mnichukue tu kama Ndugu Bill au Ndugu Branham, au lo lote mtakalo kufanya kuhusu hilo. Hilo—hilo—hilo ni sawa. Hilo ni—hilo . . . Unachoamini, shikilia wewe mwenyewe. Mwaona?

105 Na sasa, swali lingine lilikuwa nini? Nafungwa sana katika haya, nasahau mambo hayo yalikuwa nini. Moja lilikuwa, "Je, mimi ndiye yule Mwana wa Adamu?" na . . . Naamini liko hapa " . . . yule Mwana wa Adamu au ile Nguzo ya Moto ilikuwa ndiyo yule Mwana wa Adamu?" La! Ile Nguzo ya Moto ndiyo ule Upako.

106 Ile Nguzo ya Moto . . . Sasa, hili laweza kuingia kilindi kidogo isipokuwa ni baadhi yenu wanatheologia, Dk. Vayle, labda Ndugu hapo, na baadhi ya wahudumu hawa hapa toka Arkansas, na wale—marafiki wasiri wangu hapa, labda watajua.

107 Sasa, hiyo Nguzo ya Moto ndiyo ile *Logos* iliyotoka kwa Mungu. Ile *Logos*, ambayo hakika ni sifa za Utimilifu wa Mungu. Mungu alipoingia katika umbo ambapo angeonekana, ilikuwa upako wa Roho mkuu uliojitokeza, ukijidhili Kwake, ukishuka, Mungu, Baba, yule *Logos* aliyekuwa juu ya Israeli, ambaye . . . Yeye alikuwa mtakatifu, hangevumilia dhambi. Ilipaswa kuwe na toleo la damu papo hapo katika Edeni. Ndipo ile *Logos* ikafanyika mwili na kukaa kwetu; na ambapo hii *Logos* ilikaa katika mwili wa mwanadamu, ambao ulikuwa sadaka . . .

108 Mwanadamu alipofanywa kwa mfano wa Mungu . . . Halafu Mungu akashuka chini katika mfano wa mwanadamu kumkomboa mwanadamu; hilo lilileta mwanadamu na Mungu pamoja. Mbingu na nchi vilikumbatiana na kubusiana; Mungu na mwanadamu walikumbatiana kama Ubaba na Uwana wakati ile *Logos* ilipofanyika mwili na kukaa kwetu.

109 Yesu alisema, "Nilitoka kwa Mungu, nami narudi kwa Mungu." Sivyo? Baada ya kifo Chake, kuzikwa, kufufuka na kupaa, wakati mwili ule ulitwaliwa juu kuketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu . . . Sasa, simaanishi kuwa Mungu ana mkono wa kuume, Mungu ni roho. Lakini *kwa mkono wa kuume*

maana yake ni "katika uwezo na mamlaka ya Mungu." Ili kwamba katika Hilo Jina kila kitu Mbinguni kinaitwa kwa jina Hilo na kinalitii. Kila kitu duniani kinaitwa kwa Jina hilo na kulitii, Jina lililo kuu kuliko majina yote, Yesu Kristo.

110 Sasa, hii *Logos* iliyokuwa katika Yeye, ambayo ilikuwa Roho wa Mungu, Upako ule, kupitia kwa neema itakasayo ya ile Damu, akaleta wana wengi kwa Mungu, ambao wametiwa upako na *Logos* ii hii.

111 Sasa kwenye siku a Pentekoste ilishuka, hiyo Nguzo ya Moto, na ndimi za moto zilikalia kila mmoja wao, si na kujigawanya hivyo, lakini ndimi za moto zilikalia kila mmoja wao, kundi lililoteuliwa, lililochaguliwa, lililotambulishwa na hii Nguzo ya Moto, ikionyesha kuwa Mungu aliisha jigawanya Mwenyewe katika watu. Je, mnayafahamu? Mungu, yule *Logos*, akijigawanya Mwenyewe juu ya wanadamu! Mungu, si katika mtu mmoja, Yeye yumo katika Kanisa Lake lililoko ulimwenguni mwote. Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo mimi, ninyi nanyi mtazifanya pia, nyingi zaidi." Sasa, najua ile tafsiri ya King James inasema, "Kuu zaidi," lakini tafsiri sahihi ni "mtazifanya *nyingi* kuliko hizi." Mungu aliwekwa na kufungiwa katika Mtu mmoja, Yesu Kristo. Lakini sasa Yeye amewekwa na kufungiwa katika Kanisa la Mungu Aliye Hai lililoko ulimwenguni kote.

112 Hivi sasa, hali Mungu yuko hapa akinena nasi mioyoni mwetu, Yeye yuko Afrika, Yeye yuko Asia, Yeye yuko Ulaya, Yeye yuko Uingereza. Ko kote waamini wanakokusanyika, Yeye yuko papo hapo kati yao.

113 Sasa, baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kupaa na kule kuja kwa Roho Mtakatifu, Paulo akiwa njiani akienda—ambaye alikuwa Sauli—akienda Dameski, yeye aliangushwa na ile Nguzo ya Moto, ile *Logos*. Na huyo Myahudi hangeita kamwe hiyo Nguzo ya Moto, "Bwana," isipokuwa iwe alijua ilikuwa *Logos* ile ile ambayo watu wake waliifuata jangwani. Ona? Sasa, huyo hakuwa Mwana wa Adamu, huyo alikuwa *Logos*.

114 Sasa, tunasema hili kwa unyenyekevu, na upendo, na heshima. Ona? Kwamba Yesu Kristo ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, na pia katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa kabla wakati wa Lutu, au katika wakati wa Lutu kule Sodoma, ndivyo itakavyokuwa siku ile atakapojifunua Mwana wa Adamu tena, akijifunua Mwenyewe. Sasa, katika siku hizi za mwisho ile *Logos* iliyokuwa juu ya Yesu—ambapo Yeye ametoka kwa hiyo na kurudia ile Nguzo ya Moto tena na kushuka chini duniani ku-(ningesema jambo fulani, lakini natazama kanda. Hawangeamini hilo kama Ungewaambia. Haingefaa kitu. Wao. . .Watu hawangeamini, lakini nitaacha hilo)—lakini ameshuka chini kwa, kama anayechunguza hukumu inayoendelea.

115 Na sasa, hii Nguzo kuu ya Moto ambayo imethibitika dhahiri kabisa hata na kamera ya kisayansi, iliyo hapa duniani siku hizi. . . Ndiyo ile picha yake ikining'inia pale. Naamini bado iko hapo, sivyo? Je, iko pale? Imethibitishwa kisayansi na walio bora sana tulio nao. George J. Lacy, kiongozi wa Shirika la Upelelezi nchini Amerika wa alama za vidole na hati, kasema, "Niliita saikolojia, Mchungaji Branham, lakini," kasema, "ile nuru iligusa kile kioo. Niliiweka chini ya miali ya nuru zenye nguvu sana na kuifanyia uchunguzi hapa kwa siku nne au tano. Na ile nuru iligusa kile kioo. Na hiki kioo hakiwezi kupiga picha saikolojia!" Sasa, hiyo imetambuliwa.

116 Ndipo tazama kazi Zake. Ina, kati yetu, inathibitisha Yesu Yeye yule ambaye wakati mmoja aliishi Palestina, Roho yule yule aliyekuwa juu Yake amekuja kupitia kwa Mwili hata imefikia Kichwa tena, ambaye anakuja hivi punde kudai ule Mwili. Amina! Kichwa kinakuja kwa Mwili. Mnalifahamu? Huyo atakuwa yule Mwana wa Mungu, yule Mwana wa Adamu, yule Mwana wa Daudi, yule MIMI NIKO, lile Ua la Uwandani, Nyinyoro ya Mabondeni, ile Nyota ya Asubuhi.

117 Mimi si Yeye; Mimi ni mtumishi Wake. Na ile Nguzo ya Moto si Yeye; Hiyo iko katika mfano wa Roho (ona?) iliyokuwa juu ya yule Mwana wa Adamu na imekuja sasa kutia upako wana wa Adamu, kurudisha tena huduma kama tu vile Yeye alisema ingekuwa, kusudi kile Kichwa na Mwili wote uliosalia viunganike pamoja.

118 Kama tu ile—kama ile piramidi ilivyojengwa na Henoko. Nasi twaona katika piramidi hiyo, hawakuweka juu yake kamwe lile jiwe la kuweka juu. Mbona? Lile Jiwe la Kuweka Juu halijaja bado. Vile vipandio saba katika ile piramidi. . . Tutapitia hayo siku fulani, na ningetaka tu kuwaonyesha jinsi inapatana na Maandiko kikamilifu.

119 Na sasa, ukichunguza sarafu yako ya Amerika, lile Jiwe kuu la Kuweka Juu, jicho, inasema, "Ule Muhuri Mkuu." Litakuja.

Na tazama mawe hayo. . . Je, kuna ye yote hapa aliyewahi kuwa kwenye zile piramidi huko Misiri? Vema, ukitazama. . . Pale, kuna mikono iliyoinuliwa kule nyuma. Vema. Mawe hayo yamewekwa pale kikamilifu mno, na juu pale, ambapo ni kama kuba, jiwe hilo litakapokuja, itakuwa kama almasi kuu ikiingiana ndani mle kikamilifu.

120 Sasa, jiwe hilo halingeingiana chini pale juu ya huo msingi wa chini, wala halingeingiana na ule msingi wa pili au ule msingi wa tatu. Litaingiana tu na msingi wa juu wakati jengo lote limeingiana na lile jiwe. Na Yesu hawezi kuja hadi Kanisa, Mwili wa waamini na huduma ambao Yeye aliacha wakati mmoja utakuwa sawasawa na ulivyokuwa wakati huo ku. . . Ndiposa, hilo laleta. . . "Wao pasipo sisi hawatakamilika." Paulo alisema, Waebrania 11. "Pasipo sisi hawawezi kukamilika." Wao hawana

budi kupata huduma hii kuwaamsha Walutheri, Wa-Wesley, na wale wote katika nyakati zao. Wakati hiyo itakapokuja, wakati sehemu hiyo ya—ambapo tai walikusanyika . . . "Kama ulivyo mzoga ndipo tai watakapokusanyika," ndivyo lile swali lilivyokuwa. Ee, ni kamili kabisa. Natumai hayo yamelijibu lile swali.

292. Ndugu Branham, je, Shetani aweza kutumia karama za lugha au unabii katika mtu aliye na Roho Mtakatifu?

121 Hilo ni zuri, sivyo? Naam, bwana! Kama . . . Lazima ichunguzwe kwa makini mno, makini mno. Kama mtachunguza katika I Wakorintho 14:29, ninyi mnaotaka kuiandika . . . Ona? Mtu yule—yule aliyeandika hili hakuandika jina lake; walisema, "Mungu akubariki." Ona? Katika I Wakorintho 14:29 twaona kuwa karama yo yote katika kanisa yapasa ijaribiwe kwanza. Ona? Yakupasa uchunge, kwa sababu pepo wachafu hujipenyeza ndani. Kwa sababu kumbuka, mvua hunyea wenye haki na wasio haki. Mvua ile ile iliyotumwa kukuza ngano pia hukuza magugu, maji yale yale. Wangapi wajua hilo? Sasa, hilo lapaswa kudhihirisha ule uzao wa nyoka kwenu basi, jinsi huyu mwana alivyokuja. Ninajaribu kulitafuta hapa nilipate kabla wakati wangu haujakwisha lakini siwezi kulipata; kwa hivyo, jinsi mwana huyo alikuwa mzao wa nyoka. Ona?

122 Mungu ana sheria. Sasa, kuhusu hili, katika sheria hizi za Roho wa Uzima yakupasa uchunge, kwa sababu Shetani hujiingiza kati.

123 Na Paulo, kitu fulani kilipofunuliwa kwa mtu fulani, ilipasa kuwa na wapambanuzi wasiopungua wawili au watatu kabla halijasemwa mbele ya kanisa.

124 Sasa, pia hapa huenda nikatoa hili. Naona . . . Sidhani Ndugu yangu yupo hapa usiku huu, lakini mtu fulani alimfanyia mzaha mtu fulani aliyeondoka maskanini akashuka kwenda kuhudhuria kanisa la Ndugu Jackson. Kasema, "Walienda chini kule kati ya "ndege wafu!" Je, huoni aibu kutoa matamshi kama hayo? Ye yote uliye, kama wewe u mwanangu katika Kristo hapa, naona haya kwa ajili yako. Usifanye jambo kama hilo. Junior Jackson ni ndugu yangu. Don Ruddell ni ndugu yangu.

125 Vema, sababu yake ni kwamba, nilipoliweka, kanisa hapa katika hali fulani, niliporudi, kuona kama ningepata dhihirisho la karama, nusu yao waliondoka. Kwa sababu unapoanza kunena, au kuhubiri, au kitu fulani, sharti . . . Ilikuwa inafikia mahali ambapo ingekuwa vigumu kuhubiri pasipokuwa na mtu fulani aliyenena kwa lugha, mtu mwingine akafasiri, mtu fulani akatoa tafsiri; na nusu yake hata haikutimia kamwe.

126 Sasa, naamini katika kunena kwa lugha. Naamini katika kufasiri, lakini sharti iwe kitu fulani cha moja kwa moja kwa kanisa, "si Bwana yuaja upesi," au cho chote kile—ambacho

ni sawa. Lakini, "msipayuke pa yuke," kama Yesu alivyosema, "kama wafanyavyo makafiri."

127 Sharti iwe jambo fulani, "Nenda kamwambie Ndugu Fulani jambo fulani yeye alilofanya na—na . . . " Naam, nenda kamwambie Ndugu, Dada *Fulani*, yeye alipofanya jambo fulani kule chini kule majuzi, yeye aliasi sheria za mume wake—nadhiri ile kwa mumewe. Asiporekebisha hili sawa—sawa, Roho Mtakatifu atamkatilia mbali." Hapo una BWANA ASEMA HIVI!

128 Ndipo ingiza dhambi ile ndani. Hapo ndipo tunapokuwa na kanisa kama lilivyokuwa Anania na Safira walipoingia. Ndipo tuna kanisa linalosimama imara.

"Ee," mnasema, "Ndugu Branham . . . " Mtu mmoja, nilimwambia hayo; Yeye akasema; "Vema, unatufinya sana."

129 Nilisema, "Si mimi hufinywa kule na wageni ambao sijapata kuwaona maishani mwangu? Lakini nina imani na tumaini katika Mungu wangu aliyenituma mimi kufanya haya, na hakuna wakati mmoja yamekosea na hayatakosa kamwe mradi tu ni Mungu." Naam.

130 Si kunena kwa lugha na mambo kama hayo . . . Naamini kuwa lugha hizo na watu walio na hizo karama, kama wao ni Wakristo halisi na wana hamu yake, watakusanyika wenyewe pamoja, kwa sababu—na kutoa lugha zao na tafsiri na kuona kile wawezacho kufanya kuendeleza Ufalme wa Mungu. Wana huduma wao wenyewe, lakini si wa hapa katikati ya kusanyiko ambapo wenye—wenye dhambi wanashughulikiwa na kadhalika. Biblia ilisema, "Watasema ninyi ni wajinga."

131 Wakati mwingine wanakosa heshima sana nayo na—na mengineyo . . . Siyo eti kundi letu halikuwa hivyo, lakini niliwaacha waendelee kidogo. Nilisema, "Chungeni."

132 Sasa, niliwaambia hawa ndugu (kuna mashahidi hapa sasa wanaojua hili), nilisema, "Liachilieni. Baada ya kitambo kidogo nita—tutaona kama ni ya Mungu au la. Kama haiwezi kustahimili kurudiwa, basi ni mwana haramu." Hivyo ndivyo hasa Biblia ilisema. Na kurudiwa kulipokuja nini kilitendeka? Je, niliwaambia hilo muda mrefu uliopita? Ona? Mwulize mchungaji hapa.

Yeye alisema, "Na *hili* na *lile* je?"

133 Nilisema, "Liachilieni tu! Wao ni watoto. Hatuwezi kuihukumu, lakini tazama ijapo kushikilia kwa Neno hasa."

134 Sasa, Ndugu Junior Jackson alikuwa na haki ya kutokukubaliana na hayo. Yeye ataka kanisa lake . . . Watu wote wanataka kunena kwa lugha na mengineyo mkutanoni. Hizo ni taabu za Ndugu Junior; hiyo ni—hiyo ni juu yake. Lakini Junior Jackson anaamini Ujumbe huu sawasawa kama wengine wetu wote wafanyavyo. Yeye ni mmoja wetu. Na si "ndege mfu"

kuenda kule. Junior Jackson ni mtu wa Mungu ninayempenda kwa moyo wangu wote. Na hayuko hapa usiku huu, kwa hivyo naweza kumsifu nitakavyo.

135 Na—na Don Ruddell . . . Sidhani Don yuko hapa usiku huu, kwa sababu wana kanisa lao wenyewe. Lakini kama ningeona kila mtu akija humu maskanini, kisha aondoke aende kwa Don Ruddell, au—au Ndugu J.T. Parnell, au Ndugu—ye yote wa ndugu hawa humu walio ndugu zetu hapa na raia wenzetu wa Ufalme, ningefurahi sana singejua la kufanya. Ningesema, "Bwana, jaza hili tena. Hebu na tumwage hili na kulijaza tena." Ningelipenda hayo. Ningependa kuona wavulana hao . . . Wao ni—wao ni watoto wangu.

136 Sasa, J.T. au—au wengineo wote si lazima waamini tu kama vile nifanyavyo; si lazima wafanye hivyo. Kama nilivyowaambia asubuhi hii, hata mimi sikubaliani na mke wangu, au yeye hakubaliana nami. Vipi kama ningeenda mezani na Junior achukue andazi la tofaa nami nichukue andazi la tunda Ulaya. Ndugu, sisi sote tunakula andazi, tutakubaliana pale, lakini . . . Na sisi sote huhubiri Injili ile ile. Taratibu za Kanisa lake . . .

137 Mwajua, Petro na Paulo walikuwa na tofauti, si katika mafundisho yao, lakini jinsi Petro alivyokuwa akijiweka mwenyewe. Walikuwa na—na tofauti ndogo katika hilo, lakini haikuwatenganisha. Walikuwa ndugu. Naam, hakika tutakuwa na tofauti, sio tofauti . . . Sikubaliani na Assemblies of God. Sikubaliani na miongozo yao, lakini kuna watu wengi wa Assemblies of God ambao ni ndugu wapendwa sana. Sikubaliani na fundisho la umoja, lakini kunao wengi wa watu hao ambao ni watu wapendwa sana.

138 Nakubali—sikubaliani na Wabatisti, na Wapresbiteria na miongozo yao, lakini ndani mle, kuna Wakristo halisi.

139 Kwa njia yo yote jioni hii nilichukua barua ya simu. Nikaikosa. Ndugu mmoja mhubiri Mbatisti, alisema yeye ange—amekuwa akijaribu kwa muda mrefu kufikia mahali—au kupata mahali ambapo watu walimheshimu Mungu bada—badala ya kuheshimiana wao kwa wao.

140 Na ndugu mpendwa anayekuja katika kanisa hili alisema, "Nitakupeleka mahali kama hapo." Yeye alikuwa na hamu kufika hapa, Mbatisti. Mwaona, wametawanyika kila mahali. Singekubaliana na mwongozo wao, lakini hakika napenda kundi lile. Kwa hivyo usiseme hilo kuhusu hao ndugu.

141 Sasa ndani humu, karama hizi ni—ni sharti zichunguzwe. Hakuna karama . . . Lazima kuvichunguza. Shetani anaweza kuiga karama yo yote. Tazama hawa waimbaji wa Beatles sasa wakienda kuiga uponyaji wa Kiungu—watovu wa uadilifu, wachafu, waliooza, waliozaliwa toka kuzimuni. Ona? Vema.

293. Je, Danieli alikuwa mtu wa nne katika ile tanuru ya moto kwa sababu yeye alikuwa nabii katika wakati huo?

142 La, ilikuwa ni Yesu. Yule mtu wa nne alikuwa—kama Mwana wa Mungu. Sidhani alikuwa ni nabii, kwa sababu yeye alikuwa katika tundu la simba; lakini si—singeamini kuwa Danieli alikuwa katika tanuru ya moto. Ni vigumu ku—kuamini . . . Sasa, hapo huenda uko sahihi, lakini basi hilo ni wazo langu tu.

294. Ndugu Branham, katika Mwanzo 6 na kifungu cha 12, Mungu alisema kwamba kila mwenye mwili amejiharibia njia yake. Je, hili lataja kuhusu talaka na ndoa? Kama ndivyo, je, Yesu alitaja jambo lile lile Yeye aliposema kwamba "Kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu" katika Mathayo 24, kifungu cha 38 na 39?

295. Ndugu Branham, kuna watoto watakaozaliwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu—miaka elfu—Ule Utawala wa Miaka Elfu, miaka elfu ya utawala wa Kristo hapa duniani? Au kutakuwako na ishara yo yote duniani—dhambi yo yote (kunradhi) **duniani katika wakati huo; na kutakuwa na watu duniani katika miili hii wakati huo?**

143 Nitajaribu kuyapitia upesi sana. Sasa, katika Mwanzo sura ya 6, kifungu cha 12, Mungu alisema kila mwenye mwili alikuwa amejiharibia njia yake . . . Naam, hiyo ilikuwa ndoa, talaka na kadhalika. Biblia ilisema, Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, jinsi walivyooa, na kuolewa, na mambo kama hayo. Hiyo ndiyo mojawapo wa ishara za siku za mwisho, mojawapo tu wa ishara zile.

144 Sasa, kama hayo ndiyo tu ulimwengu ulikuwa ukifanya, singeliyaita ushahidi wa wakati wa mwisho, si zaidi kuliko niwezavyo kuita kunena kwa lugha ushahidi wa Roho Mtakatifu. Ni kweli kwamba hapana budi kuja wakati ambapo ndoa na talaka ziko tu kama iliyokuwa katika siku za Nuhu, lakini kuna mambo mengine yanayoandamana nalo, ni mojawapo tu ya ishara zile.

145 Na kunena kwa lugha ni mojawapo wa ishara za Roho Mtakatifu, lakini si ishara isiyoweza kukosa ya Roho Mtakatifu, si zaidi kuliko wanawake na waume wakioana na kutalikiana na kuoa tena. Hiyo haingekuwa ishara pekee. Kama hiyo ndiyo ishara pekee ambayo ingalikuwako, singeliita hivyo. Ona? Mambo mengine hayana budi kuambata na kunena kwa lugha au karama nyingine yo yote kuifanya Mungu.

146 Sasa, "Je, watoto watazaliwa katika ule Utawala wa Miaka Elfu?" Hilo ni swali moyoni mwangu, ambalo niliwaambia majuzi. Sijui. Inaonekana sana kama ingekuwa hivyo; inaonekana sana kama haingekuwa. Nitakuwa mwaminifu kwenu jinsi nijuavyo. Sijui hadi wakati huu. Kama Mungu atanifunulia hilo, nitawaambia. Lakini ngoja; lazima lije toka kwa Mungu. Ninyi mu watoto wangu. Singewaambia. Sijui kama kutakuweko au kama hakutakuweko. Siwezi kusema.

147 "...au kutakuwa na dhambi duniani wakati huo?" La! Hakutakuwa na dhambi yo yote duniani. Shetani amefungwa.

148 "Na kutakuwa na watu duniani katika hii miili ya kawaida wakati huo?" Naam, bwana! Tutakuwa na miili yetu iliyotukuzwa papa hapa duniani, tukila, tukinywa, tukijenga manyumba, na—na—na tukiishi kama tunavyoishi sasa kwa miaka elfu. Ni—ni fungate ya Bibi-arusi na Bwana arusi.

296. Ndugu Branham, Yesu alimaanishaje katika Mathayo 12, kifungu cha 32, ambapo Yesu alisema, "Ye yote atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao"? Tafadhali nifafanulie mafungu haya ya Maandiko. Asante. Na lina jina la mtu yule; yeye ni mhudumu. Vema.

149 Ndugu, mimi—wewe u mwanatheologia, mimi sivyo. Lakini ningependa kusema hili, kuwa Yesu alisema, "Ye yote atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa." Kwa maneno mengine, kuyaambatanisha na Maandiko mengine yote, "Kila dhambi watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho Mtakatifu hawatasamehewa wanadamu." Kukufuru Roho Mtakatifu ni kumfanyia mzaha, kunena juu yake, kumdhihaki, kufanya kitu kama hicho ni unapovuka mpaka kati ya mema na mabaya.

150 Sasa, ukiona Roho Mtakatifu... Kwa mfano, vipi kama Roho Mtakatifu angeshuka hapa na kupambanua kama afanyavyo, na vipi kama huyo angekuwa Roho Mtakatifu, na hukuamini ilikuwa Yeye, na uliondoka nakumfanyia mzaha na kunena juu Yake; sijali yale utakayowahi kufanya, umeangamia. Na huwezi kufanya hivyo. Hiyo yaonyesha papo hapo kuwa wewe si wa Mungu, kwa sababu Uzao wa Mungu unakaa katika mtu huyo naye hawezi kutenda dhambi. Basi dhambi ni nini? Kutokuamini. Yeye aonapo Neno likidhihirishwa, yeye ataliamini. Na yeye aweza tu...

151 Ona, kuna dhambi moja tu, dhambi moja tu. Wangapi wajua hilo? Hiyo ni kutokuamini. Naam. Kuzini si dhambi. Kuvuta sigara, kusema uongo, kuapa, hizo si dhambi. Hayo ni matunda ya kutokuamini. Unatenda hayo, kwa sababu wewe si mwamini. Naam. Kwa hivyo, ona, kuna dhambi moja pekee, na hiyo ni kutokuamini. "Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa." Haijalishi yale yeye afanyayo wala cho chote kile, yeye kwanza amekwisha kuhukumiwa. Vema.

297. Ndugu Branham, je, ni kosa kwa kijana asiyeolewa—asiyeolewa (halikusema nani) **kukata nywele zake—zao?** Nadhani ni mwanamke.

152 Naam! Ni—ni kosa kwa mwanamke ye yote kukata nywele zake. Hilo ni swali ndogo na fupi. Je, mna—mnashikwa na usingizi? Vema, tuta—tutaharakisha upesi tuwezavyo. Nilikuwa najaribu sana kupata hilo la uzao wa nyoka.

Mwombee mtoto wetu wa kiume katika . . .

Hilo ni ombi la maombi. Nililichukua tu haya na kukimbia, tu . . .

298. Ndugu Branham, je, wanawake wanaruhusiwa kufanya kazi katika mahali pa umma hali wakiwa na waume wenye afya na watoto? Ninamwulizia swali hili mtu mwingine.

153 Vema, si—si—sijui hilo. Siwezi kusema. Lakini ni—nina wazo hili. Hebu niseme hivi: Naamini, kama ningalikuwa mwa—mwanamke nami nalijua kuwa mume wangu alikuwa mwenye afya na alikuwa na kazi nzuri, anayofanya, naamini ingekuwa fu—furaha kuu kwangu kukaa nyumbani, kuwalea watoto wangu na kufanya . . . na—na—na kuwatunza watoto wangu na kuwalea, na kumpenda Bwana. Na kama ningekuwa na wakati wo wote uliosalia kwa kuosha kwangu na mambo ambayo nitakayofanya, nafikiri ningefundisha watoto wangu jinsi ya kumtumikia Bwana.

154 Sasa, kama una—deni au kitu fulani ambacho unajaribu kumsaidia mume wako kulipia, au kitu fulani ambacho kinakulazimu kufanya hivyo . . . Vema, nadhani hilo ni sawa kama utajaribu kumsaidia. Na—na uishi bibi wa heshima. Nami na—nafikiri ni vigumu. Hakuna mtu aliye na akili timamu anataka mke wake kuingia katika kundi ambamo mna wanaume watovu wa adabu, wachafu na mambo kama hayo. Lakini kama inamlazimu mwanamke kuingia katika hayo, nadhani kuwa yeye apaswa ku—mumewe apaswa kujua kuwa yeye yu Mkristo halisi anayeweza kuaminika, mwanamke mwaminifu.

155 Lakini sasa, kusema kuwa yeye hapaswi kufanya kazi si—sijui. Ona, hamna Andiko kuunga hilo mkono. Nina—ninatoa tu maoni hayo. Lakini nadhani kama mwanamke anataka kufanya kazi naye yu ataka kufanya kazi . . .

156 Sasa, mimi hakika napinga wanawake kufanya kazi katika afisi hizi ambamo hawa wafanyi biashara . . . Wanafanya yasiyofaa, wanafanya mizaha michafu. Na mwanamke mzuri na msafi akiketi pale, na mambo haya yote machafu na yenye masizi yakizungumzwa pale, hivyo, ni—ninapinga hilo. Nadhani yakupasa utoke kati ya upuzi kama huo.

157 Lakini sasa, kama mwanamke aweza kuenenda kama—kama bibi halisi wa heshima na kujaribu kumsaidia mume wake afanye kitu fulani kugharimia—nguo chache za watoto kwenda shuleni, au—au kulipa deni, au kitu kama hicho, naye ataka kufanya kazi hadi hiyo imemalizika . . . Sasa, hili si Bwana, kwa sababu sina Andiko kwa hili. Ninasema tu kuwa hilo lingekuwa maoni yangu; lakini kama sivyo, singedhani tu kwa sababu yeye ataka kufanya kazi tu na kutangatanga hapa na pale na kupata—au—pesa zaidi za kutumia, kutangatanga hapa na pale, na kukimbilia vilabu vya pombe, au kunywa pombe, kuvuta sigara, na kufanya yasiyofaa sidhani yeye apaswa kufanya hivyo.

Nafikiri yeye apaswa kukaa nyumbani, ajaribu kuwa bibi wa heshima, na kutunza nyumba yake.

299. Kama Yesu katika ya pili. . .(La!) **Kama Yesu—kama ninyi katika ndoa ya pili ambapo wote wawili tayari wametalikiwa. . .ile—ku (t-u-b-)—kutubu—ni—je, kutubu kwatosha, au mnapaswa kumaliza—au mnapaswa kukomesha uhusiano wenu wa kindoa kusudi muwe sahihi?**

"Kama—kama mko katika ndoa ya pili ambapo nyote wawili mmetalikiwa. . ." Nadhani nimekwisha jibu hilo. Ona? Naam, nimekwisha jibu hilo. Ambapo wote wawili wame—wame. . . mimi tu. . .

158 La—laiti haikutubidi kupitia kwa mambo haya, enyi watu. Nina marafiki wanaoketi papa hapa, humu kati ya hawa wanaonisikiza ninaowajua. . .Karibu tu laniva kusema hivyo, lakini si—sina budi kuyasema. Ona? Na ulimwengu uko katika hali ya uharibifu sana.

159 Maskini mwanamke fulani mpendwa anafanya makosa na kuolewa na mlevi na—na wanamwacha huyo, au maskini mwanamume fulani alioa malaya fulani bila kujua, kisha afungwe kwa huyo mwanamke au huyo mwanamume maishani mwake mwote. Hilo ni jambo la kuogofya. Ndoa ni kitu kitakatifu.

Wakati mwingi watoto wenye dhambi wanaingia na kufanya mambo, kisha wanashangaa hayo yote ni ya nini. Ni—ni ya. . . Naamini, Bwana akiniruhusu kueleza hii ndoa na talaka jinsi inavyopaswa kuwa, naamini itadhihirisha mambo chungu nzima katika hayo. Yote. . .[Mwisho wa upande wa kwanza wa kanda; upande wa pili unaanza na swali lisilomalizika—Mh.]

300. Twaona. . .Je, kwa nini hatuwezi kuuza nyumba yetu? Asante. Tume. . .(Maneno yaliyoongezwa.) **Tumeomba na kufunga—na —kuiuza, bali hamna matokeo.**

160 Vema sasa, Ndugu au Dada (hawakuandika majina yao), lakini ye yote yule, sasa, kama mnajaribu kuuza mali zenu na mmefanya kile mme. . .Mnataka kuiuza na labda mnunue nyingine au cho chote mnachotaka kufanya, sijui. Kama madhumuni yenu ni sahihi, mnajaribu kununua nyumba. . . Kama mna watoto au kitu kama hicho, mnataka kupata nyumba bora au kitu. . .Sijui habari hizo, lakini ningesema hivi: Kama mnajaribu kuiuza, na mnafunga mkijaribu kuiuza, basi likabidhi kwa Bwana na mlisahau. Ona? Kwa sababu huenda ikawa kwamba Mungu. . .Huenda mkahamia mahali penginepo, na huenda si halali. Ona?

161 Kama wewe u Mkristo na unamwamini Bwana, kwa sababu hakika wewe unamwamini au haungekuwa unafunga na kuomba. Ona? Kwa hivyo ningelilikabidhi tu kwa Bwana. Sema, "Sasa, Bwana utakapofika wakati Wako kwetu kuiuza, Wewe utamtuma mnunuzi." Ndipo imekabidhiwa kwa Bwana,

ondoa mkono wako kwake na usonge mbele. Naamini itafanyika. Ninaharakisha hapa, kwa sababu wakati unaniishia.

301. Ndugu Branham, je, ni kosa kwa mwanamke kusokota nywele zake?

162 Nimekwishajibu hilo. Hakika, sijali, iweke tu ndefu. Ona? Si...najua mna...sikusudii kuwa "mcheshi" kwenu wasichana. Ona? Hiyo ni kwa unyofu. Ninyi—ninyi—ninyi mnataka kujua, na mnaniuliza mimi. Mna imani kwangu au hamngeniuliza hilo. Sasa, nina imani nanyi, Dada, kuwa lile ningewaambia, naamini mngelifanya.

163 Siwezi kuthibitisha hilo kwa Maandiko. Kama mnataka... Kama huna nywele nzuri za kipilipili na wewe u mwanamke, unataka kuonekana mrembo kwa mumeo, kwa ajili ya mpenzi wako wa kiume, au kitu kama hicho, si—siwezi kuwaambia kuhusu kusokota nywele zenu au—au waliliita nini, kutia rangi au vipi! Si—sina lo lote la kusema kuhusu hilo; hilo ni juu yako. Mwaona? Ni nina...Ninyi tu, kati...Mwulize tu Bwana la kufanya, Yeye—Yeye atakwambia, kwa sababu ni—ninajaribu kueleza mambo kwa Maandiko. Ona?

302. Tafadhali fafanua I Wakorintho 13:8-12. Sasa kwa kuwa Neno kamili limerudishwa kwa Kanisa je, vifungu hivi vi—vimetimia?

164 Sasa, nadhani nilipitia hayo hivi punde, sivyo? "Lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika." Paulo alisema, "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, na kufanya mambo haya yote hapa...Lakini ijapo ile iliyo kamili..." Sasa, kuna cho chote kamili ila Mungu? La, bwana! Je, Mungu ndiye kamilifu? *Hapo mwanzo kulikuwako* [kusanyiko wajibu, "Neno."—Mh.] *naye Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu*. Neno bado ni Mungu. Ona? Vema, Ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika.

303. Ndugu Branham, ni kosa kunyolewa kabisa?

165 Nadhani—nadhani huyu ni mwanamume; na—natumai ndivyo. Vema sasa, wanawake wengine hufanya hilo. Hakika. Nilikuwa nikisafiri kwa wakati mmoja nilipokuwa mlinzi wa wanyama hapa. Nikienda juu hapa...Nilikuwa nimeketi mle, na mwanamume alikuwa akiongea hivyo, alikuwa amevalia kofia ya mfua chuma, nami nilikuwa tu naongea naye. Na yeye alikuwa akiendelea kuvuta sigara, alikuwa amevalia miwani ya mfua chuma imesukumwa juu hivyo. Ilikuwa juu hapa karibu Sellersburg. Nami nilikuwa nimeketi pale nikiongea na mtu yule. Yeye alisema kitu fulani pale, nasi tukaanza kucheka; nikampigapiga mguuni; nikasema, "Wee, hilo—hilo hakika lachukua keki, sivyo?"

Nami nilikuwa nimeketi pale hivyo, na—moja kwa moja—mwanamke fulani aliyekuwa ameketi upande wa pili kasema, "Niambie Ruth, unaenda ku-...?"

166 Alikuwa amevalia surupwenye, mkubwa mno, mnene kama mwanamume, ameketi pale akivuta sigara na kupumulia moshi puani mwake, nilidhani ni mwanamume. Kitu fulani kuhusu kutupa tochi yenye mwali kali ya hewa na kufanya kitu fulani, kugonga kichwa cha mtu fulani na kugonga kile *mnakiitaje*, kisha akaanza kucheka. Nilicheka pia na kumpigapiga mwanamke yule mguuni, nikidhani alikuwa mwanamume. Sikuweza kutofautisha. Huwezi kutofautisha. Na Biblia ilisema, “Mwanamke ye yote anayevaa mavazi yanayompasa mwanamume, ni chukizo.” Naam.

167 La Ndugu, ukitaka kunyolewa kabisa, nitakwambia; wewe ngoja hata ukaribie kufikia umri wangu, utakuwa hivyo. Kwa hivyo. . .Hilo ni jema. Sikusudii hilo hivyo, rafiki. Bwana akubariki kama unaamini Ndugu Branham anakwambia kweli. Sidhani Mungu anasema lo lote kuhusu wanaume, kifuniko chake—urefu wa kifuniko chake ni mradi ananyoa nywele zake. Kama yeye ataacha nywele zake zikue na ziwe ndefu kama za mwanamke, Biblia inasema ni aibu kwa mwanamume kufanya hilo.

168 Lakini sasa, kama u—mradi tu una nywele nawe u mvulana mdogo. . .Na—nami najua nimesema chungu nzima kuhusu hilo: “Nanyi, Wahuni, mlionyolewa kabisa, na kadhalika, vitu kama hivyo, lakini ni—ninasema tu hilo. Ona?

169 Si—sidhani Mungu anajali jinsi mwanamume anavyokata nywele zake, bora tu azikate, kwa sababu kichwa chake ni Mungu. Lakini kichwa cha mwanamke ni mwanamume; kwa hivyo, yeye apaswa. . .Na mwanamke akikata nywele zake, haheshimu kichwa chake. Ndipo mwanamke asiye na heshima apaswa kutalikiwa na kufukuzwa. Sivyo? Kwa hivyo mwanamke akikata nywele zake, yeye ana—mume wake ana haki kamili ya Biblia kumfukuza kwa kuishi maisha mabaya—mtu asiye mwaminifu. Wangapi wanajua hiyo ni Kweli? Ni yale Biblia ilisema, kwa kuwa haheshimu kichwa chake. Haimpasi mtu kuishi na mwanamke asiye mwaminifu.

304. Ndugu Branham, Isaya aliponena na binti wa Sayuni (au alipowaambia, nakusudia, nadhani walimaanisha “alinena juu ya”)**—wale binti wa Sayuni kuhusu vifuko, kusokota nywele, na badala ya nywele zilizosukwa vizuri, upaa; badala ya. . .Je, hayo yatakuwa ya siku hizi au je, Biblia ya kale haifai kama wengine wasemavyo?**

170 Biblia ya kale kila mara inatumika, na kila neno ambalo Mungu anasema lina maana. Naam, bwana! Jambo pekee lifanyalo toka kwa Biblia mpya hadi kwa Biblia ya kale, ni kuitukuza tu, Yesu alisema, “Mmesikia kwamba imesemwa, ‘Usizini’ (ulipaswa uwe katika tendo); lakini nawaambieni, kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Ni mambo ya kuvutia jinsi gani!

Sasa, yanipasa nifunge marafiki. Inachelewa zaidi. Sasa hilo ni ndefu mno. Hebu tuone kama naweza kupata jambo lingine. Hebu tuone.

305. Ndugu Branham, wanawake wapaswa (ole, wangu!) **kutengeneza nywele zao?**

171 Tena, kwa njia yo yote unayotaka kuitengeneza. I Timotheo 2:9. Ona? "Na wanawake wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri." **Nataka ku—nataka kutengeneza yangu inavyompendeza Mungu.** (Mungu akubariki, Dada mpendwa.) **Asante. Na Mungu akubariki. Tuombee.** Na mtu yule akaandika jina lake.

172 Sharon, hakika, Dada! Mungu akubariki. Iache ikue ndefu iwezavyo kuwa ndefu, Dada. Ni msichana mdogo. Mungu akubariki, mpendwa. Ni sawa, endelea vivyo.

306. Baada ya Bibi-arusi kunyakuliwa, je, ye yote wa wale wanawali wapumbavu ataokolewa au wao wote wataangamia?

173 La! Ona, kila kitu kitamalizika kwa ajili ya kanisa la Mataifa wakati yule Bibi-arusi atakapoondolewa duniani. Roho wa Mungu aondoka duniani: "Mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki na mtakatifu azidi kutakaswa." Kwa maneno mengine madhabahu yanajawa na moshi, ambapo yule—yule Wakili mkuu anasimama kuwatetea mahakamani. Kristo aondoka kwenye yale madhabahu; siku Zake za upatanishi zimekwisha. Kule kunyakuliwa kwaja; Yeye aondoka madhabahuni, aenda kukitwaa kile Kitabu cha Ukombozi, na kudai kila kitu ambacho Yeye amekomboa. Hakuna tena kazi ya upatanishi. Wangapi wafahamu hilo? Ninalo kwenye mojawapo wa zile Mihuri—au mojawapo wa zile . . . Naam, zile Mihuri, naamini ndiko liliko, ambapo Kristo anakuja kudai kazi Yake ya upatanishi.

174 Sasa, hebu kidogo. "Je, wale wanawali wapumbavu wataokoka." La! Mambo yote yanayotendeka yeye—yanatendeka sasa. Baada ya wakati huo yeye yumo katika hali . . . Sasa, yeye atapaswa kupitia katika ule wakati wa ile dhiki. Na sababu yake ni, ni kwa maana yeye ameukataa ule Utakaso katika utimilifu Wake. Yeye ni mwamini, anayekiri kuwa mwamini, lakini yeye atapaswa kupitia katika ile dhiki. Biblia ilisema, "Na wengine wote, yule nyoka akatoa maji kutoka kinywa chake na kufanya vita . . ." Na hiyo ni saa jinsi gani. Ile . . .

175 Hakujapata kuwa na wakati katika historia ambapo makanisa ya kawaida yamekuwa na njaa sana kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mi—mimi hunena kwa niaba ya Wafanyi Biashara Wakristo. Mara kwa mara, ni Wapresbiteria, na Walutheri, Wakatoliki, na wote wale, Wabatisti kwa mamia, Church of God, Nazarini, Pilgrim Holiness, Seventh

Day Adventist, kila mmoja wao akikuzunguka akijaribu kupata . . . Ona?

176 Sasa, hili ni jambo la kushangaza. Tafadhali msilichukue kama fundisho, lakini mwafahamu yale Maandiko yalisema yangetendeka wakati hilo litendekapo? Wakati ulikuwa umekwisha. Kwa kuwa tazama, kulikuwa na wanawali saba— au wanawali kumi walioenda kumlaki Bwana arusi na nusu yao walikuwa na mafuta katika taa zao, nusu yao hawakuwa nayo. Hiyo ni sehemu ya Mwili ule iliyokufa na sehemu iliyo hai. Wale watano wenye busara, walipo—sauti ilipopazwa, "Tazama Bwana arusi . . . " Wao wote walitengeneza taa zao— wakaamka na kutengeneza taa zao ili waingie katika ile karamu ya arusi. Lakini wakati wale wanawali waliokuwa wapumbavu waliposema, "Tupeni mafuta yenu kidogo, maana taa zetu zinazimika. (Ona?) Tupeni mafuta yenu kidogo," wao walisema, "Sivyo, tunayo tu ya kututosha sisi wenyewe. Nendeni mkajinunulie." Nao walipokuwa wakienda kununua, Bwana arusi akaja.

177 Wakati tangazo lilipotolewa, ile mbiu," Bwana arusi yuaja," kila mtu alitaka kuwa sahihi, upesi sana. Si huo ndio ule wakati ambapo maandiko yale yako kwenye ukuta.

178 "Ee, tunataka ubatizo wa Roho Mtakatifu." "Tunataka *hiki, kile* au *kinginecho!"* Lakini walipokuwa wakienda kununua Hayo, Bwana arusi akaja. Wale wenye busara wakaingia, na hao wengine wakaachwa nje ambapo watakuwa wakilia, kuomboleza, na kusaga meno.

179 Nimepata maswali malidadi ndani humu ya kuambatana na hilo: "Ni nani yule mtu aliyevalia vazi aliyeingia, ambaye hakuwa amevalia vazi la arusi?" Na maswali hayo yote yanayofungamana katika hilo.

307. Je, mtu aweza kutoa fungu lake la kumi kwa mtu binafsi, au ya yampasa Mkristo afanye kazi?

180 Hakika anapaswa kufanya kazi. Yeye ndiye mtu mmoja atakayefanya kazi, ni Mkristo.

181 "Kulipa fungu la kumi kwa mtu binafsi?" Inategemea huyo mtu binafsi ni nani? Naam. Katika Waebrania 7, wakati wa kwanza fungu la kumi lilipotajwa katika—katika hali ambayo sisi . . . Ngoja kidogo, naamini, swali nambari mbili. La! Enhee, enhee, La! Kwa Ndugu . . . Kasema, "Maswali mawili kwa Ndugu Branham."

182 Wakati . . . Katika Waebrania sura ya 7, wakati Ibrahimu alipokuwa akirudi kutoka kuwapiga wafalme, alikutana na Melkisedeki, akampa fungu la kumi. Huyo alikuwa Melkisedeki, yule Mfalme wa Salemu, ambaye ni Mfalme wa Amani, na Mfalme wa Haki, ambaye si mwingine ila Mungu Mwenyewe. Ona?

183 Lakini unapolipa sehemu ya kumi...Hakika, pale unapowiwa fungu la kumi ndipo pale unapopata chakula chako. “Leteni zaka zenu ghalani Mwangu, asema Bwana. (Sivyo?) Mkanijaribu kama anavyosema Mungu, kama sitawafungulia madirisha ya Mbinguni na kuwamwagieni baraka hata isiwepo nafasi ya kutosha.” Namhimiza mwanamume ye yote au mwanamke ambaye halipi—halipi fungu la kumi akubali hilo.

184 Ningesema hapa hata asubuhi, nikiwaambia ninyi yale yaliyotendeka nilipoona hilo, na hali gani niliyokuwamo. Lakini nikiwa mwaminifu tu niwezavyo kuwa, nilitoa sehemu ya kumi. Na nilipochukua pesa zangu mwenyewe toka kanisani humu au mikutano yangu mwenyewe, ningechukua zaidi—ningetoa sehemu ya kumi. Ndipo ningeitoa kwa wahudumu, na kutoa iliyobaki kwa wahudumu. Ndipo, wakati singeliweza hivyo, ndipo kitu nilichofanya, nilichukua asilimia kumi na kumpa Mungu tisini. Ndiposa, sheria iliponiambia singefanya hilo, ilinipasa kuchukua...Na kama ningalifanya hivyo, yote ingetolewa kwayo, basi ilinipasa kuiepuka na kutoa kwa misheni za ng’ambo na kadhalika, na halafu nichukue tu mshahara kutoka kwa hiyo wa dolla mia kwa juma; nami hulipa fungu langu la kumi kutoka kwake.

185 Naam, bwana! Naamini katika kutoa fungu la kumi. Ni mojawapo wa baraka za Mungu ambazo zimethibitishwa kuwa baraka. Mnasema, “Hilo ni la Agano la Kale.” Ni la Agano Jipya pia! Naam, bwana!

308. Mpendwa Ndugu Branham, mtoto akizaliwa wa—nje ya ndoa, je, mtoto huyu aweza kuokolewa au kuwa katika kule kunyakuliwa?

186 Kuokolewa? Naam, hakika, naamini mtoto yule ange-... huyo Mtoto hawezi kuzuia lile limekwisha kufanyika. Hiyo ni kweli. Lakini ni...Kuhusu kuwa katika kule Kunyakuliwa... Kuokolewa, ningesema, “Naam.” Lakini katika kunyakuliwa ni mzao aliyechaguliwa tangu awali aingiaye katika kule Kunyakuliwa. Na siwezi kuamini kuwa wa uzinzi alikuwa mzao uliochaguliwa tangu awali. Mwafahamu? Ona? Naamini watu wanaweza—mtoto yule anaweza kuokolewa; hana—hana haki yake mwenyewe. Ni tendo mbaya mno na kadhalika.

187 Lakini sasa, katika Agano la Kale mtoto alipozaliwa mwana haramu, hata hangeingia katika kusanyiko la Bwana kwa vizazi kumi, miaka mia nne na kitu, laana hiyo ilikuwa mbaya mno. Wazia hilo. Mtoto asiye na hatia, mjukuu wa kining’ina cha kining’ina cha kining’ina chake, waza tu, kining’ina cha kining’ina cha kining’ina, vining’inia kumi vya mtoto yule hata hangeingia katika kusanyiko la Mungu. Naam.

188 Lakini mwaona, hakukuwa na lo lote pale lenye nguvu kutosha kusamehi dhambi hiyo. Ile damu ya Agano la Kale haikusamehe dhambi; ilizifunika. Lakini ile Damu ya Yesu

Kristo huiondolea mbali. Hiyo ndiyo tofauti sasa. Damu ya Yesu Kristo inapoingia, hiyo ndiyo tofauti.

309. Ndugu Branham, tunataka kuwa karibu na Ujumbe wako iwezekanavyo. Je, tuhamie Arizona au Jeffersonville?

189 Jiamulieni, mojawapo. Hakika nawapenda, sijali mnaenda wapi, mnafanya nini. Lakini sasa, kama wosia, naamini ningekuja Jeffersonville. Kama mtahama haidhuru, ningekuja Jeff. Naamini mimi niko hapa zaidi kuliko nilivyo Arizona. Hilo ni zuri.

310. Ndugu Branham, je, ku—kumechelewa zaidi kuhubiria tena wenye dhambi?

190 La! Hasha! Usiingize hilo niani mwako, Ndugu. Endelea kujenga nyumba. Endeleeni kufanya kila mwezacho. Endeleeni hata mtakapotwaliwa. Ona?

311. Swali nambari 2. Je, waliookoka wapaswa kujitenga na wenye dhambi katika ibada? Je, waliookoka wanapaswa kujitenga na wenye dhambi kuabudu?

191 Sijui hasa lile unalomaanisha. Kama unamaanisha wenye dhambi kule nje kwa...Unamwabudu Mungu kila mahali. Lakini nadhani kama tungefanya hivyo, tutapataje kanisa, kwa sababu wenye dhambi huja kanisani na kuketi kando ya Mkristo. Usijitenge na cho chote ila dhambi, si wenye dhambi. Mchukue mwenye dhambi ukiweza, lakini usiwe mshirika katika dhambi zake.

312. Je, mke aliyeokoka apaswa kujinyima kwa mume wake kama mumewe ni mwenye dhambi?

192 La bwana! La, bwana! Huyo ni mumeo. Utampeleka mbali sana na Mungu kuliko alivyowahi kuwa kwa kufanya hivyo. Ona? Naam, Ndugu, Dada. Uliolewa naye; naye ni wako, nawe ni wake.

313. Ndugu Branham, nini maana ya kutangua ndoa? Je, watu wale wako huru kuoa au hili ni jina tu la talaka? Ningependa maelezo machache juu ya hili.

193 Hakika wameoana. Mradi tu wametoa hiyo nadharia, wameoana. Ni kama tu kwa mvulana, kama mvulana anaahidi msichana kwa nia njema, yeye ana wajibu kwa msichana huyo. Yeye ni kama tu aliyemwoa. Jambo pekee sheria ifanyalo, ni kuwapa ninyi hati ya—ya haki ya kuishi pamoja kama mume na mke. Lakini mwanamume anapomwambia mwanamke, "Nitakuoa, Mpenzi; nitakuchukua wewe kama mke wangu. Je, utanikubali...?" yeye ameoa.

194 Nadhiri yako ni takatifu, hiyo ndiyo ikuozayo haidhuru. Hakuna mhubiri awezaye kuwaoza, wala hakimu, wala cho chote kile, ni nadhiri yako mwenyewe kwa Mungu na mwanamume huyu. Unapoahidi, umeolewa.

195 Tazama. Unasema, "Ndugu Branham, je hilo...? Ulisema ungejibu hilo kwa Biblia." Je, mnataka Biblia kwa hilo? Inueni mikono yenu mkitaka. Sasa, tuna dakika karibu sita au nane. Vema.

196 "Yusufu, mumewe, akiwa mtu mwenye haki (mumewe aliyemposa, tayari aliitwa mumewe)...Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu mwenye haki, alikuwa 'akiazimia' kumwacha kwa siri kwa ajili ya haya; lakini kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. (Ona?) Na Malaika wa Bwana akamtokea katika ndoto akisema, 'Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua, Mariamu, mkeo." Amekwisha oa, yeye alikuwa amemwahidi.

197 Na ya...Na bi mdogo, kama uliahidi kumwoa mvulana yule, una wajibu kufanya hivyo. Ukimwoa mwingine baada ya nadhiri hiyo, basi, tangu sasa na kuendelea haidhuru—utakuwa ukiishi katika uzinzi. Na tazama, jambo lile lile kwa mvulana anayeahidi kumwoa mwanamke...

198 Usitoe nadhiri yako kwa mtu ye yote isipokuwa umekusudia kuitimiza. Kumbuka, kuna Biblia kwa hiyo. Yusufu aliahidi kumwoa Mariamu. Na Mungu alisema kuwa hilo lilikuwa...

199 Soma sheria za Agano la Kale kuhusu hayo. Ona? Torati ya Agano la Kale, kama uliahidi kumwoa mwanamke, na ukamwoa mwingine, ulikuwa ukizini; na ulifukuzwa nje ya marago. Naam, bwana! Yakupasa utimize nadhiri zako unapoahidi mwanamke hilo. Yeye ni chombo kidogo kitakatifu, nacho ni cha kuleta uhai wa watoto duniani tena. Kwa hivyo unapomwahidi, yakupasa umwoe.

314. Je, kumechelewa sana kwa ibada za gerezani na kazi kama hizo kwa ushuhuda kujaribu kuwaokoa watu? Pia mtu apaswa kuuza vyote walivyo navyo sasa, kwa sababu Bwana yuaja upesi?

200 Vema, una—unafanyaje...Natumai sijasema lo lote ambalo lingewafanya ninyi kuamini mambo hayo. Sivyo? Kama nimefanya hivyo, nisameheni! Sikukusudia...Ona? Msibahatishe tu mambo hayo. Endeleeni, hubirini, muwe na ibada gerezani, mkimtolea kila mtu, na usi-...

201 Tazama hapa. Wa-Seventh Day Adventisti hapa si muda mrefu uliopita, yapata miaka hamsini au sitini iliyopita, nililiona katika gazeti la *Courier-Journal* (ninalo mahali fulani sandukuni), sehemu kubwa mno ya gazeti la *Courier-Journal*, ambapo walitupilia mbali mabawa ya kale, ambapo walipokuwa wakiitwa Millerites kabla wao hawajakuwa Seventh Day Adventist. Na walikuwa na kipande chote kikubwa cha karatasi katika gazeti la *Courier* juu hapa Franklin, Kentucky, wakati wote walipouza mali zao na kupata...Waliweka tarehe fulani, wakaithibitisha kwa Maandiko—Yesu alikuwa yuaja kwa tarehe hiyo—na kuenda juu pale na kutwaa vinubi vyao na kadhalika,

na kuketi juu ya mlima. Asubuhi iliyofuata wakashuka, umande ulikuwa umewalowesha na manyoya yao yote yamepukutika, nao walishuka wameishiwa pumzi. Ona? Ni kundi la kidini lililojitenga na kadhalika.

202 Msiamini hilo. Yesu huenda asije kwa miaka mia. Sijui Yeye atakuja lini. Hakuna mtu ajuaye Yeye atakuja lini! Lakini nitajaribu kuendelea kuhubiri na kufanya kila kitu niwezacho hata Yeye ajapo. Kama hayuko hapa leo, nitakuwa nikimtarajia kesho. Kama Yeye hayuko hapa ku—juma hili, nitakuwa nikimtarajia juma lijalo. Kama Yeye hayuko hapa katika miaka kumi ijayo, na ningali hai, nitamtarajia katika miaka thelathini ijayo. Ona? Bado nitamtarajia. Sijui Yeye atakuja lini, lakini nataka kuishi mwaminifu kwa Neno Lake na mwaminifu kwa watu Wake, na kuishi kama Mkristo, na kungoja kule kuja Kwake. Ona?

203 Endelea kuhubiri ibada gerezani kumfanya kila mtu mwezaye aokoke. Sijui Yeye yuaja lini, hakuna ye yote ajuaye. Lakini nitasema jambo hili moja. Hii ndiyo sababu ninajaribu kuwaambia ninyi, nami natumai hamjaribu kuweka tafsiri yenu wenyewe. . . Si kumshambulia mtu huyu. Mungu, kubariki Ndugu, Dada, ye yote yule. Ilionekana kama alikuwa mtu fulani toka nje ya mji huu, kwa sababu ilikuwa kwenye—kwenye kadi ya posta badala ya barua, nadhani, toka Denver, Colorado, na. . . Naam, Pike's Peak, Colorado. Kwa hivyo huenda ikawa mtu fulani aliituma hapa kwa posta, lakini hiyo hilo ni kamili hasa. Huenda wakapata kanda.

204 Lakini hebu tukumbuke, usigeuze lo lote, ila tu njia yako ya dhambi kuendea haki. Endelea tu kwenye kazi yako, ukiendelea tu vivyo hivyo. Wote wanaofahamu hilo semeni, "Amina!" [Kusanyiko wajibu "Amina!"—Mh.] Ona? Fanya hilo sasa!

315. Ndugu Branham, katika Mathayo 12:40, inasema, "Kama vile Yona alivyokuwa katika—siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi." Inawezekanaje kuwa siku hiyo wanayosema—siku hizi ambapo wao husema Yeye alilazwa kaburini Ijumaa jioni na akafufuka Jumapili asubuhi, ikifanya tu usiku muwili na mchana mmoja?

205 Sasa, ukichunguza ilisema, "Kama ilivyokuwa" (mwaona?) katika siku ambapo Yona alikuwa katika tumbo lile kwa siku tatu usiku na mchana. Ni kati ya siku tatu na usiku na mchana, kati ya hizo tatu usiku na mchana, kwa sababu huwezi kufanya Maandiko yadanganye. Nabii alisema, "Sitamtoa mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitakuachia kuzimu nafsi Yake." Na uharibifu huingia katika mwili wa mwanadamu katika masaa sabini na mawili, ambayo ni siku tatu usiku na mchana. Wakati

fulani ndani ya hizo siku tatu usiku na mchana. ndipo—Yeye angefufuka toka kaburini.

206 Kwa hivyo kuwa siku tatu usiku na mchana halimaanishi yapasa iwe hivyo hasa; ni wakati fulani ndani ya hizo siku tatu mchana na usiku. Yeye alipaswa kufufuka, kwa sababu unabii hauwezi kuvunjwa, kwamba ile . . . Yeye hangeona uharibifu na ungeona uharibifu kama Yeye angekaa kwa wakati huo hasa.

316. Ndugu Branham, kama mwanamume ameoa na kutaliki (si hilo ni baya mno (ona?), mengi sana? Sasa, sisemi lo lote dhidi ya watu; hilo tu liko mawazoni mwa watu. Hakika, wanasumbuliwa. Kule kunyakuliwa, watu hawakuwa wakiwaza sana kuhusu hilo; hayakuwako mambo mengi sana kwake. Lakini sasa, yametandaa ulimwengu. Na watu husoma mambo haya katika Maandiko. Na watu, walio wateule, nje kule wanakuja kutazama hilo. Nao wanaliona, nao ni wanyofu. Wanataka kujua. Hiyo ndiyo sababu nataka kulijibu kwa busara nyingi sana niwezayo kuwapa ninyi)**—ameoa na kutaliki kisha akamwoa mwanamke mwingine ambaye pia ameolewa na kutalikiwa na ndipo akaolewa naye, na hawa wawili wana—wana—wameoana machoni pa Mungu—je, hao wameoana machoni pa Mungu? Wote wawili au mmoja wao awezaje kunyakuliwa?**

207 Vipi? Sijui. Singewaambia. Swali ni, "Je, wao waweza kuwa katika kunyakuliwa?" Kutalikiwa, kila mmoja wao ametalikiwa, kila mmoja wao ana mwenziwe aliye hai, ndipo wao walioa tena, wote wawili walioa na kuoana tena. Na sasa, yule ambaye . . . Mwanamke huyu ana mume aliye hai; mwanamume huyu ana mke aliye hai. Na sasa, wana watoto na kadhalika na wanataka kumjia Mungu. Je, wao wanaweza kuenda katika kule kunyakuliwa? Hilo litakuwa juu ya Baba wa Mbinguni. Singejibu hilo. Ona?

208 Nili—niliona jambo moja. Biblia ilisema wao wataitwa wazinzi. Na Biblia ilisema pia, "Mzinzi hataingia katika Ufalme wa Mbinguni." Hilo ndilo lote niwezalo kusema. Ni—ninajua, hilo laniva tu kusema hilo, lakini siwezi kusema ila yale Neno husema. Yanipasa kukaa nalo. Natumai kuwa hayo yote sivyo yalivyo. Kuna mahali mbalimbali katika Biblia . . .

209 Sikushauri wewe. Tafadhali, hebu nikupe tu Andiko ndogo. Tafadhali, tafadhali usi—usi—usi . . . Kama unaishi kwa furaha na mume wako, unaishi kwa furaha na mke wako, tafadhali baki hivyo. Je, uta—uta . . .? Kwa sababu niliwaambia hilo, msi—msiwaache hao watoto wadogo bila nyumbani na mambo kama hayo. Mungu amerekebisha katika mahali ambapo watu wa—wa—walifanya mambo vibaya. Mnakumbuka, Yesu alisema kuhusu Daudi alipokuwa na njaa, kwamba aliingia katika hekalu la Mungu na kula ule mkate wa wonyesho, ambao ni halali tu kwa kuhani, na anapatikana asiye na hatia. Kuhani pia

kakufuru Sabato katika siku ya Sabato na wanapatikana wasio na hatia, na mkuu kuliko Sabato alikuwa hapa. Ona? Pale... Mimi...Hebu tuli—hebu tuliachie Mungu, na kuendelea, na kuishi tu jinsi mna...Mwi—mwishieni Kristo tu sasa.

210 Hebu tuone, huenda kukawa nafasi kwako kuingia. Msifanye...Makosa mawili hayatafuta moja. Endeleeni kuishi jinsi mlivyo kama m—kama mna furaha pamoja. Huenda ukawa na mwenzio asiyekupasa. Nitasema jambo hili moja: kama una mwenzio asiyekupasa katika mke huyu—katika maisha haya, hautakuwa naye katika yale mengine. Makosa yote yatarekebishwa

317. Je, waamini wote waliozaliwa mara ya pili watanyakuliwa?

211 La, waliosalia tu, ni wale waliosalia tu, si waamini wote waliozaliwa mara ya pili. Biblia ilisema, "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie miaka elfu," na ndipo wao walifufuliwa na kubaguliwa, kondoo kwa mbuzi. Si waamini wote waliozaliwa mara ya pili wataingia katika...kulingana na Maandiko.

318. Nini ishara mathubuti kuwa mtu hakika amejazwa na Roho Mtakatifu?

212 Yohana 14:26: Ata-... "Lakini huyo Roho Mtakatifu ajapo (ona?), atawaonyesha mambo yote yajayo." Ona? Ata-...Yeye atayakamilisha; "yaliyotengenezwa na mwanadamu" hayatafaa kitu; na Yeye ni Neno. Huyo Roho Mtakatifu ajapo, Yeye atajitambulisha Mwenyewe ndani yako kwa Maandiko. Na hiyo ndiyo ishara halisi kuwa Roho Mtakatifu yumo ndani yako, kwa sababu Yeye ni Neno.

213 Sasa tazama! Vipi kama ulinena kwa lugha? Nataka tu kuwauliza ninyi hilo. Yesu alisema Roho Mtakatifu ajapo Yeye angefanyaje. Na vipi kama ulinena kwa lugha, ukaruka juu na chini, ukapiga shangwe, na cho chote kile, halafu uje kwa Neno; nami ningewaambia ule ubatizo wa—niwathibitishie ninyi kwa Maandiko kama nilivyofanya, kuwa ubatizo kwa kutumia vyeo vya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni kukosa kufahamu kabisa Maandiko—hakuna ye yote aliyewahi kubatizwa hivyo—na mnaendelea na kuyashikilia haidhuru? Je, ungeniambia Roho Mtakatifu ndani yako angefanya jambo kama hilo? Awezaje kukana Neno Lake mwenyewe?

214 Ninapowaonyesha yale yanayopaswa kutendeka katika siku hizi, jinsi Mwana wa Adamu apaswa kujifunua Mwenyewe, na yale Yeye apaswa kuyafanya, na Maandiko haya yote ambayo yamekuwako sasa, na ndipo kumwona Yeye akishuka moja kwa moja chini na kujitambulisha, na mnashikilia dhehebu na kusema mmezaliwa mara ya pili? Je, unaweza kuona busara hapo?

215 Je, ningemwambia mke wangu ninampenda, na niwe na mpango na mwanamke mwingine, na kuzurura hauku na

huko, na ndipo kumwambia mke wangu kwa moyo wangu nampenda? Je, wadhani huo ungekuwa upendo halisi? Je, yeye angeniambia ananipenda, na hali ninapoondoka, yeye akimbia na mwanamume mwingine?

216 Hivyo ndivyo hasa Israeli ilifanya ku-. . .Unajua Biblia pale, jinsi Yeye alisema, kasema. . .Israeli, kasema, "Mmepanua paja zenu na kumchukua kila mwanamume anayepita, na mmenifanyia ukahaba, nami nitawataliki katika talaka." Hakika! Hiyo ni nini? Unatenda uzinzi dhidi ya mwili wako mwenyewe. Na mwanamke aondokapo na kuishi na mume mwingine, au mwanamume na mwanamke mwingine, na tayari wameolewa, wanachafua miili yao wenyewe. Na mtu asemapo yeye ni Mkristo na atakana kabisa Maandiko kuwa ni Kweli, yeye anazini dhidi ya Mwili ule ambao yeye anadai kuwa ndani yake. Ona? Kwa hivyo ni chapa ya mpinga Kristo, sana hata ingedanganya Mteule kama yamkini.

319. Ndugu Branham, ni haki kwa m-mtoto mchanga kuvaa suruali ndefu na suruali fupi?

217 Mchanga vipi? Acha tu wewe uwe mwamuzi wa hilo; kama wewe ni Mkristo. Msichana mdogo au mtoto mchanga, nadhani, sijui, mimi. . .Jambo pekee nijualo, Biblia yasema ni chukizo kwa mwanamke kuvaa mavazi yanayo—yampasayo mwanamume. Ona? "Mwanamke," haikusema, "mtoto." Lakini sasa, nina. . .Jiamulie mwenyewe kuhusu hilo, mimi. . . Kwa upande wangu, sioni kosa lo lote kwa mtoto mdogo, msichana mdogo wa umri wa miaka minne au mitano akiwa. . .Wanapokuwa watoto wadogo, mwajua lile nakusudia, wanakimbia hapa na pale kule bustanini. Kama yeye amevaa, kile unachoita suruali ndefu au cho chote kile, ni mtoto mdogo, si—sioni lo lote baya kwalo. Labda. . .

218 Ona, ninawaambia tu yale Neno lisemayo. Ni chukizo kwa mwanamke kuvaa mavazi yanayompasa mwanamume.

320. Tutakusanyika wapi pamoja? Nawe ulisema tukusanyike pamoja kwa zile Parapanda.

219 Naamini, samahani, Dada, ye yote yule, ume—umekosea pale. Sikusema kamwe mkusanyike kwa ajili ya zile Parapanda. Nilisema Israeli walikusanyika kwa Parapanda, si Bibi-arusi wa Mataifa. La, la! Zile Parapanda, kulia kwa zile Parapanda Saba kulikuwa kwa kukusanya Israeli (wangapi wajua hilo?) toka kote. . .Naam, si. . .La, la! Ee, jamani! La, la—si—si Israeli. Kwa hivyo, si hivyo. . .Hatukusanyiki kwa Parapanda zile na yule—kule—yule Bibi-arusi hakusanyiki kwa hizo. Parapanda zitakuja baada ya Karamu ya Pentekoste. Ona? Na kunyakuliwa kwaja. . .Na hilo. . .si swali hili sasa.

321. Ndugu Branham, kama una wakati tafadhali fafanua Mathayo 10:41. Nataka nijue nini thawabu ya nabii?

220 Vema sasa, Yesu alisema, “Ampokeaye nabii kwa kuwa ni nabii, hupata thawabu ya nabii.” Thawabu ya nabii ni kuwa rafiki wa nabii. Ampokeaye mwenye haki kwa kuwa ni mwenye haki, hupata thawabu ya mwenye haki. Sivyo? Na wakitaka kujua thawabu ya nabii ni nini, ni kuwa rafiki wa nabii. Ona? Hiyo ni thawabu. Yeye ni rafiki yenu.

221 Kama yule mwanamke Mshunami, huenda ikakufaa wakati mmoja. Ona? Ilimfaa yule mwanamke. Ona? Watazame watumishi wa Mungu.

Ee, Jamani! Sasa, tuna. . . Ya—yanipasa tu nimalize na, rafiki ni—ninachukia kulifanya, lakini tazama hapa, tazama yale, mamia. [Ndugu Branham asihiwa na Kusanyiko ajibu zaidi—Mh.] La! Lakini—najua, lakini ona, ni—nafurahiwa ninyi mkisema hilo, lakini ninawaza kuhusu maskini watu hawa ambao bado wataendesha motokaa zao mamia ya maili usiku huu. Lo, hayo yako mengi sana ndani mle, nina-. . .

322. Ndugu Branham, ningependa kujua kuhusu ule Utawala wa Miaka Elfu. Je, ni baada ya ile Karamu ya Arusi, au—au itakuwa duniani, habari zake zote. Nina—sifahamu hilo.

222 Vema, Ndugu, au Dada, ni vigumu kwangu kuufahamu pia, mimi binafsi. Ila tu jambo niwezalo kusema ni hili: kuwa ile Karamu ya Arusi inakuja kabla ya ule Utawala wa Miaka Elfu.

223 Sasa ona, mtu fulani, najua mahali fulani ndani humu ana swali juu yake, lililosema “Ndugu Branham, ume—umekosea kwa yale majuma sabini ya Danieli. Bado kutakuwa na majuma sabini.” La, Masihi alipaswa kuja na kuhutubu, na katikati ya lile juma la sabini, juma la sabini, ambalo ni miaka saba, Yeye alika—Yeye angekatiliwa mbali kati ya walio hai na kufanywa dhabihu. Wangapi wanakumbuka hilo? Vema. Yesu basi alihubiri kwa miaka mingapi, yule Masihi? Miaka mitatu na nusu. Basi bado kuna tatu na nusu iliyokusudiwa.

224 Na katika Ufunuo sura ya 11, hawa manabii, wanatabiri kwa siku elfu moja mia mbili na sitini. Miaka mitatu na nusu bado imeahidiwa Israeli wakati yule Bibi-arusi wa Mataifa atakapoondoka. Wangapi wanafahamu hilo sasa? Ona? Vema, vema.

323. Hili ni. . . nina kiosk cha chakula cha mchana nami huwatumikia watoto wa shule ya sekondari kwa sehemu kubwa. Tangu kuingia katika Nuru, nimeondoa mitambo ya kucheza kamari pamoja na ile (ule mtambo wa santuri wa kutumbukiza ndani pesa) **mtambo ule nimeuondoa. Vijana wale huvuta sigara nao wanataka muziki wa rumba kwenye—kwenye redio. Naifungua tu kwa karibu masaa manne kwa siku. Si—siungi mkono kuvuta sigara au kunywa pombe, lakini naogopa kushikilia mahali pale.**

225 Mnajua hiyo ni shida. Ona? Jambo ni kwamba una—una huenda inakupasa kujipatia riziki. Lakini unajua hilo

lingenifanyiaje mimi? Hilo lingenipa fadhaa singeweza . . . Ni—ni hilo . . . Huenda ukaweza kuyastahimili hayo, lakini hilo kundi ndogo la "Wahuni" ndani mle wakitenda yasiyofaa, na hao "Hawara," Ninge—ninge—lingenipa wazimu. Ona?

226 Na nakuambia; ni—nina . . . Kama ingekuwa yangu, najua kile ningefanya. Ningesema, "Komesheni hilo au ondokeni hapa." Ona? Ningeendesha mahali pazuri au nisiendeshe po pote. Lakini wewe, kama inakupasa kuifanya kwa riziki, sitaki kukudharau wewe, Ndugu au Dada. Ni—ninajua ni vigumu kusema mambo haya; lakini hilo—hilo tu . . . Si sahihi (mwaona?), kwa sababu lilionekana kama . . .

227 Kama mtu fulani alivyosema asubuhi hii kuhusu wanawake wetu kuvaa nguo zao fupi sana, wanawake wetu walio wazima, walikuwa mfano mbaya kwa wasichana. Nadhani hilo ni hivyo pia. Mwaona?

228 Nami nadhani vivyo hivyo. Wanapokuona wewe mle ndani ambamo mna huku kuvuta sigara kwote na kutenda yasiyofaa, na wanajua ushuhuda wako, na huku kulaani kwote na—na watoto wadogo wanawazunguka hivyo, nao wakiendelea hivyo, nawe husemi lo lote kuhusu hilo, ni jambo baya kwa ushuhuda wako. Fanya lo lote Bwana akuongozalo kufanya. Naomba ya kwamba Mungu atakuongaza kwa njia sahihi.

324. Kama (k-u-s-i-) kusimama mustarini kuingia Kanisani kutakuwa tu jambo la kukumbukwa, kipi kitatendeka kama hatutapitia katika ile dhiki? Je, sisi tuta—tutapata—vivyo hivyo—mateso madogo? Kama hatutaona . . .

Ona? Mimi . . . Swali hili labda ni hili. Ninajaribu kuenda upesi; si—si—sipaswi kufanya hivi. Yanipasa kuweka hili nyuma kwa sababu kuna mahali ambapo ungeweza kukaa kwa hili kwa saa moja (ona?) na lina—kulichambua. Nita—nitakoma.

229 Tazama. Watu wanataka kusema hilo, wakidhani kuwa wao—Kanisa litaingia kwenye ile dhiki? Ona? Halitaingia; haliwezi (ona?), kwa sababu limekwisha kombolewa.

230 Sasa, kanisa, wale—wale waamini wa kidesturi kama Lutu, atapitia katika ule wakati wa ile dhiki (ona?) na kuokolewa kama kwamba ilikuwa kupitia kwa moto. Nuhu alipitia katika ile dhiki, akainuliwa juu yake, akaokoka pamoja na Hamu aliyeichafua nchi tena. Ona? Lutu aliokoka, binti zake wenyewe walilala naye, na akapata watoto kwa binti zake. Ona? Lakini Ibrahimu alizaa ule Mzao wa Kifalme, alizaa yule Mzao wa ahadi. Henoko alienda katika kule kunyakuliwa, alitembea tu akaenda nyumbani. Yeye hakupitia katika ule wakati wa ile dhiki iliyo kuu. Mwaona?

231 Naam. Ona? Halikosi, Biblia haiwezi kwa mfano . . . Na mifano haiwezi kukosa kutimia. Ona? Haibashiri kuwa yule Bibi-arusi . . . Sasa, kanisa litapitia katika wakati wa ile dhiki.

232 Sasa watu husema, "Itakuwaje kwa wale watakatifu wa kale?" Huo ulikuwa ugeuzo wa majira. Hilo lilikuwa chini ya mateso, ambayo kama mngekuwa hapa kusikiza hizi *Nyakati za Kanisa*, na kuona jinsi walivyoingia katika giza na walipaswa kufanya hivyo, ndipo hilo laonyesha ambapo iliwapasa kupata mateso hayo, kwa sababu kila moja ya nyakati saba za kanisa na kila kitu kinaanza kuonyesha kuwa zilikuwa giza na kuzidi kuwa giza zaidi, hata mwishowe wakafikia mahali kabisa ambapo walikana Jina Lake na kuchukua jina lingine kuwa wako hai na hali wamekufa, Sardi. Na ndipo likajitokeza, Thiatira na Sardi, na ndipo kukaja—ndipo ikaanza kufikia Filadelfia na kadhalika, kisha kukaja wakati wa kuita yule Bibi-arusi atakayeepuka hukumu zote. Alihesabiwa kuwa amestahili kuepuka hukumu hii yote na gadhabu ijayo juu ya dunia, ili uweze kuhesabiwa kuwa umestahili kuiepuka, si kusipitia humo, kuiepuka. Ona? Je, mwafahamu sasa, kila mtu? Ona?

233 Kanisa, lile vuguvugu, lo lote lile nje ya yule Bibi-arusi mteule litapitia katika ule wakati wa ile dhiki iliyo kuu. Hawatafufuka katika ule ufufuo wa kwanza: "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu," wale tu waliochaguliwa tangu awali, walioteuliwa asili, Bibi-arusi mteule, uteuzi wa Mungu Mwenyewe. "Ni nani, Ndugu Branham?" Sijui? Siwezi kuwaambia ni nani, lakini najua watakuwako, kwa sababu Bwana alisema wangekuwako. Ona? Ni wao ndio wale watakaoinuliwa juu toka kwa ile dhiki, lakini wengine wote watapitia katika ile dhiki, waangamizwe, na kila kitu kitaauawa kabla ya ule Utawala wa Miaka Elfu. Ndipo wale—wale wenye haki watatokea katika ule Utawala wa Miaka Elfu na waishi miaka elfu.

234 Na baada ya hiyo miaka elfu, ndipo ule hukumu wa kile Kiti cha Enzi kikubwa, Cheupe, itakapokuja, na ndipo wafu, wote wenye haki na wasio haki watafufuliwa. Na vitabu vile vinafunguliwa, na kile Kitabu cha Uzima kikafunguliwa; na watakatifu, yule Mke na Mume, waliketi na kuuhukumu ulimwengu. Na ule msemo utatimia: "Na Yeye atawahukumu mataifa kwa fimbo ya chuma." Mataifa yote yatasimama mbele Zake pale, naye atawahukumu wao kwa fimbo ya chuma. Yeye atawabagua kondoo na mbuzi na kuwaambia mbuzi, "Ondokeni," na kondoo, "Njooni, enyi mliobarikiwa na Baba Yangu."

235 Sasa ndipo, kutakuwa na mkutano wa kampi wa watakatifu juu ya mapana ya nchi. Na Shetani anafunguliwa toka gerezani na aende kufanya vita tena na watakatifu, vivyo hivyo alivyofanya Utukufuni hapo mwanzo. Na ndipo Mungu atanyesha mvua na viberiti toka mbinguni, na dunia yote inaondolewa kama. . .Itateketezwa na kuangamizwa. Na hakuna tena bahari, hakuna tena maji, hakuna tena cho chote

kilichosalia duniani. Volkeno itapuliza na kuvuja na kulipuka, na kitu hicho chote . . .

236 "Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya: kwa maana mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita; wala hapana bahari tena. Nami, Yohana, nikauona Mji ule Mtakatifu ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu kama Bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe." Mwaikumbuka? Na katika huyu Bibi-arusi . . . "Tazama Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu," na Mungu atakaa pamoja nao juu ya huu Mji unaofanana na piramidi wa maili elfu na mia tano mraba. Na juu ya Mji huo kutakuwa na Nuru. Amina!

> Ee, mji huo juu ya Mlima Sayuni,
> Ijapokuwa mimi ni mgeni, bali ningali naupenda.
> Nitakutana nawe katika nyakati hizo,
> Nifikapo kwa mji huo juu ya mlima ule.

237 Juu ya Mlima Sayuni yule Mwana-Kondoo ataketi. Na Mji ule hautahitaji nuru, kwa kuwa yule Mwana-Kondoo atakuwa Nuru humo. Na juu ya Mwana-Kondoo atakuweko Baba, ambaye ni *Logos*, Mungu, yule Nuru kuu, ile Nuru ya Milele itaangaza juu tu ya kile Kiti cha Enzi. Na Yesu hatakuwa juu ya Kiti cha Enzi cha Baba, Yeye atakuwa juu ya Kiti Chake cha Enzi. Na Baba atavuma juu ya Mwana, ambapo Baba na Mwana watakuwa Mmoja. "Na wakiwa katika kunena, nitajibu. Kabla hawajawaza, ninawawazia!" Naam.

238 Naye Yesu ataukabidhi wakati mkamilifu, mkamilifu kwa—Mungu mkamilifu aliye hai, ambao Yeye amewakomboa na kumkabidhi Baba. Sivyo? Atageuka kuwa Mungu Baba ambaye ni Roho, si mwanadamu, Roho. Maumbile yote ya uzuri yamekusanyika pamoja, hayo ni Mungu. Na katika wema . . . Sasa, lo lote lililopotoshwa toka kwa wema ni ovu; huo ni ufalme wa Shetani. Mema yote ni ya Mungu. Uovu wote ni wa . . .

239 Ndiposa Mungu akafanyika kitu cha kuonekana katika Mwanadamu aliyeitwa Yesu Kristo, ambaye alikuwa Mwanawe. Huyu Mwana aliutoa Uhai Wake kusudi apate kuwaleta wana wengine, kusudi Mungu apate kuwa wa kugusika, akifanya kazi katika wote ndani ya wote. "Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba Yangu, na Baba ndani Yangu, Nami ndani yenu nanyi ndani Yangu."

240 Ee, ndugu, hiyo itakuwa siku yenyewe kweli. Haitakupasa kuendesha toka kule Birmingham kusikiza Ujumbe; Ujumbe utakuwa pamoja nasi wakati huo, sivyo? Ee, itakuwa—itakuwa wakati wa ajabu, ajabu mno. Tunatarajia siku hiyo; na Mungu ailete upesi.

241 Huo Mji mkuu unaoketi pale (sasa, ona?), hauta . . . Mnadhani, "Urefu wa maili elfu moja na mia tano kwenda juu?" Hivyo ndivyo Biblia ilisema. Sasa, hautakuwa maili elfu moja na

mia tano kuelekea juu hali umenyoka hivyo. Ona? Tuna kipimo kingine cha kigeografia kwamba pande zote ni sawa; hiyo ni piramidi. Ona?

242 Na Mji ule utaanza labda karibu na mwinamo wa sitini kipimioni. Na ukianza, maili elfu moja na mia tano ya huo, waza tu jinsi huo utakavyokuwa mrefu, lakini itachukua muda gani kuwa pale. Itakuwa vigumu kujua unapanda mlima. Kwa maili elfu moja na mia tano juu kwa mwinamo wa sitini kipimioni, uko tu karibu hivi. Ona? Na Mji ule wote uko juu ya mlima huu. Na una kina sawa na urefu; ni urefu sawa na upana. Urefu, kwa kina, kwa upana, vi—viko sawa; kuta zote ni sawa. Piramidi ina kuta nne, na hizi kuta nne zitakuwa . . .

243 Sasa, kuta zile za kuuzunguka Mji ule zitakuwa—zitakuwa na urefu wa futi 216, dhiraa 144, na kila moja yayo ni jiwe. Waza tu kuhusu Mji huo, marafiki. Lo, jamani! Sababu gani—gani tunaketi hapa katika hapa mahali pa joto? Mbona twafanya mambo haya? Mbona tunaendesha hivyo? Mbona tuna—mbona tunasumbuka? Huo unastahili kila inchi ya njia.

> Ee, masumbuko ya njiani hayataonekana kama kitu,
> Tifikapo mwisho wa njia.

Naam. Na, jamani, utakuwa wakati jinsi gani.

244 Na pale Yesu ataketi kwenye kile Kiti cha Enzi. Na nje toka chini ya kile Kiti cha Enzi utatiririka ule mto wa Uzima, ukitiririka chini ya hizi kuta nne hadi katika ufa mdogo, na katika vijito vidogo hata vikawa mto, na ukatelemka katika Mji ule. Utatiririka chini barabarani hivyo, na pande zote kuna miti ya uzima itakayozaa—au kugeuza matunda yao kila—kila baada ya siku thelathini. Ee, ni Mji jinsi gani.

245 Na kumbuka, Mungu, aliye Muumba mbingu na nchi, yuko Utukufuni hivi sasa akiutayarisha Mji huo. Ibrahimu aliutarajia. Yeye aliondoka nyumbani mwake; akatengana na kila kitu kilichokuwa kizuri kwake na kuutafuta . . . Mbona? Yeye alikuwa nabii. Na akiwa nabii, yeye aliunganishwa na Roho na sehemu ya Roho yule. Na kitu fulani kilimwambia toka ndani yake, "Kuna Mji," naye akaanza kuutafuta. Kasema, "Mimi ni msafiri, na mgeni. Ninautafuta Mji ambao Mwenye Kuubuni na Kuujenga ni Mungu." Yeye alijua Mji huo ulikuwa mahali fulani. Ee, lo! Nami naamini papo hapo kwenye ardhi ile ambapo yeye aliutafuta, mumo humo Palestina, hapo ndipo utakaposimama, kwa maana uko kwenye Mlima Sayuni. Hapo ndipo Huo—utakapokuwa.

246 Tazama mahali utaenea na kufikia ile—ile bahari, toka bahari hadi bahari. Fikirini kuhusu huo Mji wa maili elfu moja na mia tano mraba ukiwa nje pale milimani mwa Bwana. Ee, huo utakuwa wa ajabu!

247 Na simba na mwana kondoo watalala pamoja. Simba atakula nyasi kama ng'ombe. Na dubu atakuwa mpole, na

mbwa-mwitu atafugika. Utakuwa wakati jinsi gani! Hakuna cho chote kitadhuru wala kuharibu; kila kitu kitakuwa na amani na upendo. Hakutakuwa tena na uzee; hakutakuwa tena na magonjwa, wala kufa.

248 Wenzangu, hii si hadithi ya Baba Krismasi, kitu fulani cha kutungwa, imeandikwa katika Neno. Na Neno halijawahi kushindwa. Hebu wazeni juu ya ahadi ile ya . . . Si nyuma katika siku za Biblia, lakini katika siku hizi, siku ile ambayo Mungu— leo. Hakuna yodi moja imekosa kamwe kwa Neno Lake. Ee, naelekea kwenye Mji huo. Naupenda, nanyi je?

249 La! Sasa, Ndugu, Dada, yasema saa tatu na dakika ishirini. Najua nina marafiki kadha hapa toka Kentucky. Najua nina marafiki hapa toka mahali mbalimbali nchini. Mkitaka kukaa usiku wote, nitalipia vyumba vyenu. Niliwaambia, na chakula cha jioni kinawangoja na kuwalipia hoteli kama mlitaka kukaa. Na jambo pekee likupasalo kufanya ni kumwona nyuma kule, na hakika nitalifanya. Nitafanya lo lote niwezalo kuwasaidieni ninyi. Nawapenda.

250 Sikusudii kuyajibu maswali haya labda wakati mwingine kinyume. Kama hauliamini, hilo ni sawa kabisa. Nawatakeni mnipende vivyo hivyo, kwa sababu Mungu ajua nawapenda ninyi vivyo. Nayajibu maswali haya tu kadiri nijuavyo—huenda nilikosea katika baadhi yake, marafiki, lakini haikukuwa kwa kupenda kukosea. Kama ningekuwa na kama maswali sita au manane hivyo, ningekaa moja kwa moja na kuyafafanua, lakini mimi, badala ya kuyapitia yote . . . Nina machache yayo kuhusu ndoa na talaka. Nilikuwa tu—nilidhani ningejibu machache yake. Sikupata mengine zaidi yamewekwa hapa, kuyachukua, lakini nina maswali muhimu mno hapa, maswali muhimu mno. Nataka kuwajibia ninyi nikiweza.

251 Sasa, kama unaishi hapa karibu, mwite Billy, Jumatano, nitajua wakati huo kama nitarudi. Nitaomba juma hili. Lakini nina mahojiano mengi ya kibinafsi, ee, tita karibu *hivi*. Nami nina mambo mengi *hivi* kule Arizona ya kufanya hivi karibuni nikiweza. Na ni watu ambao ni wagonjwa mno. Baadhi yao wana shida, nao hawajui la kufanya—waume na wake wenye shida.

252 Na baadhi ya haya hapa yalipaswa kuwekwa kwa mahojiano ya kibinafsi, kwa sababu singeyasoma moja kwa moja, yale wale watu walisema ndani humu kuhusu mambo yao ya ndoa na mambo kama hayo. Nami nilimwambia Billy arudi na aone ni akina nani, na—na awaite, na kuwaambia tutayaweka tu kwa mahojiano, ili niweze kuongea nao. Baadhi yake ni mazito mno, na maswali yapaswayo kujibiwa.

253 Niko hapa kujaribu kuwasaidia, kwa sababu nawapenda. Ninyi ni watoto wangu niliomzalia Kristo. Nadai kila mmoja wenu. Nadai ninyi usiku huu; nadai ninyi wakati wote; mimi kila mara huwadai ninyi kisha—kama ndugu yangu na dada. Ninyi ni

watoto wangu; mi—mimi ni baba yenu katika Injili, si baba kama vile kasisi angalikuwa, mimi—mimi ni baba yenu katika Injili kama Paulo alivyosema pale. Nimewazaa ninyi kwa Kristo, na sasa na—nawaposea ninyi Kristo; hilo ni kufanya ninyi muweke nadhiri ya ndoa kwa Kristo kama bikira wasafi. Msiniaibishe! Msiniaibishe! Ninyi iweni bikira safi.

254 "Nitalifanyaje hilo, Ndugu Branham?" Kaa moja kwa moja na Neno; ishi msafi na mwadilifu; usiwe na uhusiano wo wote na ulimwengu. Kama upendo wa ulimwengu uko moyoni mwako, sema, "Ee, Yesu, tafadhali ondoa huo toka kwangu. Sitaki kuwa hivyo."

Sasa sikusudii kuwa tu mtu anaye—anayesema hili. Ni—ninakusudia kuwa mwamini halisi. Kumwamini Yesu Kristo na kumwishia Yeye kila siku. Usifanye maovu.

255 Sasa wakati mwingi ninanena kuhusu imani ya Kikalvini. Sasa, usidhani hilo lakuachilia ufanye lo lote unalotaka kufanya. Mtu mmoja hivi majuzi . . . Nilisema, "Je, ulienda kanisani."

Yeye akasema, "Nilienda kuwinda."

Mke wa mtu yule alinijia, naye alikuwa anatoka kufua nguo siku ya Jumapili. Nami nikasema, "Mbona hukuenda kanisani?"

Yeye akasema, "Nilienda kufua nguo."

Nikasema, "Haingekupasa kufanya hivyo."

"Vema," yeye kasema, "Mimi si maskini mfuata sheria."

Nilisema, "Lakini nilidhani ulikuwa Mkristo." Ona? Nilisema, "Je, ulijua unaweka kikwazo mbele ya mtu mwingine." Ona? Nilisema, "Linge- . . . "

"Vema, ahaa, ni—ninaamini *hivi*. Hainipasi kufanya mambo hayo. Mimi si mfuata sheria."

256 Vema tazama Ndugu yangu, Dada, tazama hapa. Paulo alisema, "Iwapo kula nyama kutamkwaza ndugu yangu safarini, hakika sitakula nyama hata milele." Nami nadhani lingekuwa bora zaidi . . .

257 Sasa, mwasema "Ndugu Branham, unawinda. Je, uliwahi kuwinda Jumapili?" Hebu niwaambieni kitu fulani. Si—Mimi sijisifu mwenyewe kwa jambo hili, lakini nina . . . Mimi si mwadhimisha Sabato sasa, naamini Roho Mtakatifu ndiye Sabato yetu. Naamini hilo, lakini naamini yatupasa kuheshimu kule kufufuka kama ukumbusho. Huo ni ukumbusho kuwa mimi . . . Kama unaadhimisha siku yo yote, adhimisha kule kufufuka.

258 Sasa hakuna sheria yo yote ya kuadhimisha siku fulani, kwa sababu unaingia katika Sabato ya amani, unapoingia ndani Yake. Nina swali hilo kujibu ndani humu hivi karibuni haidhuru, Bwana akipenda, kuhusu ni ipi siku ya Sabato? Nitaifafanua. Mungu akipenda.

Na sasa tazama, kumbuka hili. Ona? Nilipokuwa mtoto mdogo, juu papa hapa ambapo Eichs aliishi kwenye ile barabara, nilikuwa na umri wa karibu miaka kumi na minne; nilikuwa najipatia riziki kwa kuwinda. Kitu pekee nilichokuwa nacho kusaidia kupata chakula katika nyumba yetu ilikuwa kushika nyegere, cheche, komba.

Napenda kutega, na ilinipasa kufanya hilo. Ningeenda shuleni nikinuka kama nyegere, nami—mimi nilikuwa tu na jozi moja ya nguo, na hizo tu ndizo ningevaa. Hizo tu ndizo nilizokuwa nazo. Mama angenichukua na kuziosha, nikazivaa tena; na sasa, hivyo ndivyo nilienda shuleni, mvulana mdogo. Lakini nilikuwa nimesimama pale usiku mmoja; nikasema, "Nimetega mitego juu pale karibu kwa Wathen, kule juu." Ningeondoka kila asubuhi karibu saa nane usiku nikiwa na taa ya mafuta kuangalia mitego hii, ndipo nirudi wakati unaofaa kwenda shuleni. Ningeshika sungura; ningemwuza kwa senti kumi na tano. Ningepata kijisanduku cha risasi toka kwa hizo, na labda hizo zingewaua sungura watatu au wanne. Zile hatukutumia kukoka biskuti na sungura—naam, na mchuzi wa chakula cha jioni, ningeuza zingine, na labda kupata za kutosha kununua mkate, au chakula kidogo, au unga wa kutumia kutengenezea mchuzi. Sijui kama iliwabidi kuishi hivyo au la.

259 Ningeweka nyavu mtoni; niende kule chini na kupata samaki, na kuwauza kwa senti kumi kwa ratili. Kutega nyavu zangu. Sikuwa na mtumbwi; ningeelea juu ya gogo. Niingie mtoni—na ungali baridi—kuweka ndoo ya chambo nje hapa kwenye gogo lile na ku—kupiga kafi na kupiga kafi hivyo, mwili wangu uchi mtoni, na kuendesha hili . . . Nilikuwa na kamba upande huu, kufungia samaki wangu. Hao samaki wa kale wakinichoma-choma kwa pezi mguuni mwangu wakienda hivyo, na kuweka chambo Yangu kwenye . . .

260 Lakini tazama, usiku mwingi nimeenda mtoni kule saa tano na kutikisa kila kipande cha chambo kwenye ugwe. Kama singeshika samaki wa kutosha katika siku sita, sikutaka zile zilizokuja siku ya saba. Nimesimama pale katika mvua.

261 Usiku mmoja naweza kujiona mimi mwenyewe ningali nimesimama, nikiegemea kwenye . . . Nilikuwa mwenye dhambi; lakini nilikuwa nimesimama, nikiegemea kwenye kikingi hivi, mlangoni. Ee, mvua ilikuwa ikinyesha, karibu saa tano. Nilisema, "Nitachelewa usiku huu, lakini ninaenda kutangua kila mojawapo wa mitego hiyo. Sitamshika kwenye siku ya Sabato." Nilisema, "Sita—sitaitega mitego hiyo." Mungu aliliheshimu hilo.

262 Nakumbuka wakati ule ambao kila mara nilitaka, kila mara, maishani mwangu mwote nilitaka kuwa mwindaji. Baba yangu alikuwa mwindaji. Mwajua, nyanya yangu alitolewa risavuni; naye alikuwa akipata malipo ya uzeeni. Napenda tu kule nje.

263 Nami nakumbuka mimi kila mara nilitaka. . . Ni—nilitaka maishani mwangu mwote. . . Nilidhani kama ningeweza kupata pesa za kutosha hata niwe na bunduki muundo wa .30-30. . . Kama ningeweza kuipata, wakati huo ningenunua mitego kadhaa. Ningeenda milimani; ningeacha mengine ya ulimwengu yapite. Niliwaza, "Labda wakati fulani ningechukua bunduki yangu .22 na kufanya mazoezi ya kuwa mlenga shabaha bora, mwindaji fulani wakati mwingine angetaka niandamane naye. Kama ningekuwa mlenga shabaha bora, yeye ataniruhusu niandamane naye kwa ajili ya ulinzi wake; nitapata nafasi kwenda kuwinda." Nazitazama, zikining'inia kutani mwangu, zile bunduki bora sana ambazo pesa zingenunua zinaning'inia pale, hata naweza kuwaazima watu bunduki waende kuwindia.

264 Yeye huniruhusu kuingia milimani na kuhubiri, na baadhi ya waongozaji bora walioko ulimwengu hunipeleka kuwinda, bila malipo. "Neema ya ajabu, ni tamu vipi ikitamkwa."

265 Nilipokuwa. . . Hata asubuhi hii, mwindaji kulungu mzee hapa mahali fulani aliye na bunduki muundo wa .35 Remington—hakika sikuihitaji bunduki hiyo kweli—lakini yeye alinikumbatia, kasema yeye anazeeka sana kwenda kuwinda, "Nataka kukupea wewe bunduki yangu." Niliwazia nilipokuwa mvulana mdogo, jinsi, kama ningeliwazia nilikuwa na bunduki kama hiyo, jamani, ingekuwaje. Na sasa, nawaza tu, zikining'inia kwenye ukuta, bunduki nzuri sana, na mahali pa kwenda kuwinda.

266 Nakumbuka nilipoenda kule nje, na wavulana wale wangenunua aisi krimu. Na wakati mwingine baadhi yao wangekuwa na senti iliyobaki na wangeninunulia moja. Lo, singeliwanunulia nao moja. Niliwaza, "Laiti ningeli-. . . "

267 Nao wakati mwingine walikuwa wakinunua hizi za kale, tunazoziita "sambusa ndege." Sijui kama ninyi nyote mwakumbuka au la, lakini baadhi yenu watu wa kale. . . Unaipata kwa senti moja, ina chungu nzima ya vitunguu vilivyokaangwa ndani yake. Ee, napenda vitu hivyo. Tulipokuwa wadogo hatukuwa. . . Ugali tu na mboga—mnajua jinsi ilivyo—kukula.

268 Sasa mtu fulani angeninunulia mojawapo wa sambusa hizo, lo, jamani, ningelamba vidole vyangu nilivyoishikia. Ilikuwa—ilikuwa ladha nzuri sana. Nami niliwazia, "Jamani, mtu huyo, laiti ningelimnunulia sambusa." Na sasa, naweza kununulia kanisa chakula chao cha jioni.

269 Nakumbuka mambo hayo yote, na yote yalitoka wapi? Neema ya Mungu, hakuna lo lote nililofanya.

270 Nakumbuka nilitembea barabarani hapa na nikaongea na mtu fulani. Baba yangu—ninyi nyote mnajua—yeye alikunywa pombe; yeye alitengeneza pombe. Na kamwa—hakuna ye yote aliyenijali. Ningepitia barabarani na kujaribu kuongea na

watu; bado mimi hukutana nao siku hizi. Kujaribu kuongea na mtu fulani, kama hakuna mtu mwingine kuongea naye, wangesimama, "Naam, enhee, enhee." Ona? Nilikuwa wa Branham.

271 Kwa hivyo, ningekasirika mno, na kugeuka, na kuondoka. Niliwaza, "Mimi sina hatia ya hilo. Sikufanya yale babangu alifanya. Sikuwahi kamwe kunywa pombe maishani mwangu. Kwa nini yanipasa kukabiliana na hayo?" Nami nilikuwa nikimwambia mke wangu hapo si muda mrefu umepita, "Karibu yanipasa nikae nje ya mji." Mungu ameshakuwa mwema kwangu.

272 Nilikumbuka ambapo yeye alimwambia Nathani akiketi pale wakati mmoja. Nathani. . .Daudi alisema, "Je, ni haki kwangu kuishi katika nyumba ya mwierezi na sanduku la agano la Mungu wangu liko chini ya hema nje pale." Yeye . . .

Nathani, nabii yule, alisema, "Daudi, fanya yote yaliyo moyoni mwako, maana Mungu yu pamoja nawe." Huyo Nabii alifanya kosa, si kwa kupenda.

Usiku huo Bwana akamjia huyo nabii, kasema, "Nenda kamwambie mtumishi wangu Daudi, 'Nalikutwaa katika zizi la kondoo, ukichunguza kondoo wachache nje kule; nami nimemfanyia jina kama jina la wakuu walioko duniani. (Hakuwahi kusema alimpa jina kuu mno, Yeye alimpa tu jina kama watu wakuu waliokuwa duniani.) Nimekufanyia mambo haya yote, Daudi. Nimewakatilia mbali adui zako ko kote ulikoenda. Nimekuwa pamoja nawe. Sijawahi kukosa kukushindia, nami sitakosa kukushindia. Lakini sitakuruhusu ujenge mji ule.'"

273 Niliwaza kuhusu hilo, mahali sasa ambapo Mungu amenisaidia na kunifanya nijue watu wakuu, akaniruhusu niende ulimwenguni kote. Na watu toka ulimwenguni kote wakipiga simu waje niwaombee, na watu wagonjwa, na—wanataka dakika chache nawe, ambapo miaka michache iliyopita hata hawangegeuka—wangegeuza vichwa vyao wakiniona barabarani. Na sasa, wafanyi biashara wananufaika kwa watu ninaoleta mjini na nilio nao hapa, kwa vyakula vyao na gharama zao za mahoteli, na mambo kama hayo, ime—kuenda mahotelini na kote mjini na mambo kama hayo.

274 Watu ambao. . .Watu hawakunipenda kamwe; hakuna ye yote aliyenijali. Na sasa, kwa msaada wa Mungu, naamini kuwa ninamuongoza Bibi-arusi wa Yesu Kristo. Ee, "Neema ya ajabu, ni tamu vipi ikitamkwa."

275 Ilitoka wapi? Elimu yangu? Sina yo yote. Ilitokea wapi? Utu wangu? Sina wo wote. Je, ilitokana na kujua kwangu thelogia? Sijui yo yote. Ilitoka wapi? Neema ya Mungu iliyoniokoa.

Ni neema iliyoufundisha moyo wangu uchaji,
Ni neema inayotuliza uoga wangu;
Neema hiyo ilionekana ya furaha vipi,
Saa ile niliyoamini kwanza.

Kupitia kwa hatari nyingi, masumbuko, na tanzi,
Nimekwisha kuja;
Ni neema iliyonileta salama umbali huu,
Neema ile itanipeleka nyumbani.

Na tukisha kuwa kule katika
Mji huo miaka elfu kumi,
Unaong'aa kuliko jua;
Hatuna siku chache za kuimba sifa Zake,
Kuliko tulipoanza kwanza.

Ee, jinsi ninavyompenda Yesu, hilo Jina la ajabu lililoniokoa nilipokuwa mwe—mwenye dhambi, lililoniponya nilipokuwa mgonjwa, linaloniahidi makao katika Mji huo. Nina nyumbani katika Mwamba huo. Hakuna kilicho muhimu sasa ila kuwakusanya watoto wote wa Mungu pamoja na kusema, "Haya twendeni." Ile saa, inafikia usiku wa manane; kumechelewa zaidi ya tunavyodhani. Hebu na tuombe.

276 Bwana Yesu, kuisha kwa siku kamilifu. . .Kama tungelisimama juu ya mlima na kulitazama jua, wakati ile miali miekundu inapochomoza kwenye milima mikubwa ya magharibi kule, lije jicho kuu linapojifumba lenyewe, ndege wanaanza kuelekea kwenye viota, usiku unakuja. Tumeona siku nyingine kuu ya Kiroho wakati Roho Mtakatifu amekuwa akitusaidia kujibu maswali haya. Sasa, tunaenda kwenye viota vyetu, Bwana. Utulinde; usiache lo lote lituguse, Bwana. Tulinde na wale nyoka wa usiku na maovu. Na Mungu awe karibu nasi wakati wote, akitulinda na kutusaidia.

277 Naomba, Baba wa Mbinguni, kuwa Wewe utabariki kila mtu aliyekuwa mkutanoni, wale ambao hawangehudhuria, wote wanaosikiza kanda hizi. Na maswali haya yasiwe mazito sana. Na kama nimefanya kosa, Bwana, Wewe wajua moyo wangu; sikulikusudia. Naomba, Mungu, kama kuna lo lote baya, kuwa Wewe hutaliacha kamwe, hutaliacha kamwe liendelee; na kanda ikome. Usiniache nimdanganye ye yote, Bwana. Na mimi niwe mtumishi Wako mwaminifu, kwa maana hiyo ndiyo hamu ya moyo wangu wote. Au ninaishi au ninakufa, au ninangoja au ninaendelea, au ninalala au nimeamka Yeye ajapo, haijalishi kwangu, Baba, mapenzi Yako yatimizwe. "Kwa kuwa najua ya kuwa Mteteaji wangu yu hai, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi hii. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, lakini pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mungu." Huyo alikuwa nabii Ayubu wakati alipoona kule kuja kwa Bwana.

278 Pia Bwana, leo kama watumishi Wako, tunatarajia na kuona kuja Kwako. Kwa hivyo haijalishi kwetu, Bwana, lini, vipi, wapi. Tunataka tu tukupendeze Wewe. Sisi tuko mikononi Mwako. Tuhifadhi, Bwana, hata jua litakapopambazuka. Liruhusu, na ndipo sisi sote tutapiga hatua kuelekea Sayuni katika Mji huo ambapo Mwana-Kondoo ndiye Nuru.

279 Watoto wangu wapendwa humu, Bwana, niliokuzalia Wewe kwa pingu za Biblia, wao ni tunda la Neno hili. Wananipenda, nami nawapenda. Nami najua kuwa Wewe unatupenda sisi sote. Twaomba, Mungu, kuwa utatujaza mno mimba ya Neno Lako hata tumwone Yeye pekee. Liruhusu, Bwana. Na tujazwe mno Neno Lake hata Roho aweze kututumia ko kote na mahali po pote kudhihirisha Neno lo lote ambalo Yeye ameahidi. Tujalie hayo yote. Hapa kwa kusanyiko hili hapa hizi . . .

280 Ndugu yangu Jackson anarudi sasa, kule Afrika Kusini. Enda pamoja naye na mke wake; uwe pamoja hao, Bwana. Waongoze safarini mwao.

281 Hapa kuna Ndugu Lee Vayle anaandika, akiandika kila neno ninalosema, akijaribu kutengeneza kile kitabu. Ee, Mungu, wasaidie Ndugu Vayle na Dada Vayle.

282 Hapa kuna ndugu toka kule chini Ar—Arkansas, na—na wale wana wa Martin, na—na—ndugu hawa wengine. Naomba kuwa Wewe utakuwa na kila mmoja wao.

283 Uwe pamoja na Ndugu Neville, Ndugu Capps, Ndugu Ruddell, Ndugu Jackson, wote. Ee, Mungu, ni wengi mno. Wametoka Georgia, toka Alabama, na kote nchini na ulimwenguni kote. Tunawaza kuhusu ule wimbo:

> Ee wanakuja toka Mashariki na Magharibi;
> Wanatoka kwenye nchi za mbali;
> Kula pamoja na Mfalme wetu,
> Kula kama wageni wake, (Yeye amewaalika kumla Yeye. Binafsi)
> Wasafiri hawa ni heri jinsi gani
> Wakiutazama uso Wake mtakatifu,
> Unaong'aa kwa upendo wa Kiungu;
> Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
> Watang'aa kama vito vya thamani katika taji Yake.

284 Ee Mungu, na sisi tung'ae sana kama vito vya thamani katika taji Yake, ili wengine waone na wawe na hamu ya kumtumikia Yeye. Tujalie, Bwana. Walinde barabarani. Bariki kila mtu.

285 Na Baba, kwa wakati wako uliokusudiwa . . . Mimi ni mtumishi Wako. Kama unataka mimi niendelee na haya juma lijalo au kuwa na mahojiano hayo, nifunulie, Bwana, na nijue kati ya sasa na Jumatano ili tupate kufahamu. Tujalie, Baba, kusudi watu waweze kuja. Nami naomba baraka hii kwamba

utatusaidia sisi na—na ukutane nasi tena hapa kwa mkutano wetu mwingine unaofuata.

286 Uwe na Ndugu Neville na wanaume hawa wanaoleta Neno kule Texas, na Arkansas, na mahali mbalimbali; uwe tu pamoja nao, Baba. Ndugu Peary Green na kundi lile lote pale, na—uwe tu pamoja nao wote, Bwana; wao ni watoto Wako wadogo. Kila mahali ulimwenguni kote wanangoja kuja Kwako. Tusaidie sisi, Baba tunaomba, tunapojikabidhi wenyewe Kwako. Katika Jina la Yesu tutumie. Amina.

287 Napenda wimbo huo, *Wanakuja Toka Mashariki Na Magharibi*. Wangapi wanaujua? Sijui kama ninaujua, lakini nadhani najua kifungu kimoja. Huenda ukaufuatia, Dada. Sijui kama wao wanaweza kuupata.

Ee, wanakuja toka Mashariki na Magharibi;
Wanatoka kwenye nchi za mbali,
Kula pamoja na Mfalme wetu,
Kula kama wageni wake,
Wasafiri hawa ni heri jinsi gani.
Ee, wakiutazama uso Wake mtakatifu
Unaong'aa kwa upendo wa Kiungu;
Washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Watang'aa kama vito vya thamani katika taji Yake.

Ee, Yesu yuaja upesi;
Majaribu yetu yatakwisha wakati huo.
Ee, itakuwaje Bwana wetu akija wakati huu
Kwa wale walio huru toka kwa dhambi.
Ee, je, ingekuletea furaha,
Au huzuni na fadhaa.
Bwana atakapokuja Utukufuni,
Tutamlaki juu hewani. (Mnaupenda Huo?
Hebu tuujaribu tena.)

Ee, watakuja toka Mashariki na Magharibi;
Ee, wanakuja toka nchi za mbali,
Kula pamoja na Mfalme wetu,
Kula kama wageni Wake,
Wasafiri hawa ni heri jinsi gani.
Wakiutazama uso Wake mtakatifu,
Unaong'aa kwa upendo wa Kiungu;
Ee, washiriki waliobarikiwa wa neema Yake,
Watang'aa kama vito vya thamani katika taji Yake.

Ee, Yesu yuaja upesi.
Majaribu yetu yatakwisha wakati huo.
Ee, itakuwaje Bwana wetu akija wakati huu
Kwa wale walio huru toka kwa dhambi.

Ee, je, lingekuletea furaha,
Au huzuni na fadhaa,
Bwana wetu katika Utukufuni ajapo,
Tutamlaki juu hewani. (Wangapi wanataka kumlaki Yeye kule juu? Lo, jamani!)

Ee, Yesu yuaja upesi; (Hebu fungeni macho yenu na muwaze mioyoni parapanda itakapolia.)
Shida zetu zitakwisha wakati huo.
Ee, itakuwaje Bwana wetu akija wakati huu
Kwa wale walio huru toka kwa dhambi.
Ee, je, ingekuletea furaha
Au huzuni na fadhaa?
Bwana atakapokuja Utukufuni,
Tutamlaki juu hewani. (Mnapenda hilo?)

288 Pat uwe na moyo wa ushujaa! Kutapambazuka kwa ajili yako hivi karibuni. Sikuona ilienda wapi, lakini ilionekana nzuri. Amina! Una wakati mrefu, Ndugu, itarudi. Na kama mkate juu ya maji itakurudia siku moja. Ndivyo. Naam.

Ee, mnampenda?

Yesu kwa imani,
Nakutumaini,
Peke Yako;
Nisikie sasa,
Na kunitakasa,
Hivi nitaweza
Kufuata.

Hapa nazunguka
Katika mashaka,
Na matata;
Palipo na giza
Utaniongoza
Nami nikwandame
Siku zote! (Je, hampendi hayo?)

Yesu kwa imani,
Nakutumaini
Peke Yako;
Nisikie sasa,
Na kunitakasa
Hivi nitaweza
Kufuata.

Kibarikiwe kifungo (Ee, lo!)
Kitufungiacho mioyo,
Ushirika wetu wa fikira zetu
Ni kama ule wa Mbingu.

Mbele ya enzi ya Baba,
Dua zetu twaziomba;
Hofu zetu na matumaini yetu,
Hayo ni mamoja kwetu.

Tutawanyikapo,
Hiyo yatufadhaisha;
Lakikini tungali pamoja rohoni
Hata tutakapokutanika.

289 Dada Wilson, unakumbuka yapata miaka thelathini na mitatu au miaka thelathini na mitano iliyopita katika mkutano mdogo nyumbani tungeshikana mikono? Nilijua unakumbuka hilo. Ee, hebu tunyoshe mikono sasa na kushika mkono wa mtu fulani aliye karibu.

Kibarikiwe kifungo
Kitufungiacho mioyo,
Ushirika wetu wa fikira zetu
Ni kama ule wa Mbingu.

Mbele ya enzi ya Baba,
Dua zetu twaziomba;
Hofu, na matumaini yetu,
Hayo ni mamoja kwetu.

Tutawanyikapo mbali,
Hiyo yatufadhaisha;
Lakini tungali pamoja rohoni,
Hata tutakapokutanika.

Je, mnapendana? Watoto wadogo, pendaneni.

Hata twonane huko juu,
Hata twonane Kwake kwema;
Hata twonanehuko juu,
Mungu awe nanyi daima.

290 Mnampenda? Je, si Yeye ni wa ajabu? Mnapendana? Nyosha mkono, mwambie mwingine kitu fulani. Sema, "Mungu akubariki, Ndugu. Akubariki, Dada."

291 Wanatusikiza usiku huu ng'ambo ya mto kule, Dada Wilson. Naweza kumwona mzee Ndugu Seward akitembea sakafuni, akipiga makofi. Nilimwona ndugu yetu nyuma kule akiwa na ndevu kwenye uso Wake akiinua mikono, akimsifu Mungu; nikamkumbuka Ndugu Ryan, jinsi yeye alivyokuwa akiketi papo hapo mle ndani katika yale maskani ya kale akiwa na ndevu ndefu hivi. Yeye anasikiza usiku huu ng'ambo ya yale malango ya Utukufuni, mtakatifu mpendwa wa kale. Si Yeye ni wa ajabu?

Peleka jina la Yesu
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako.

Thamani na tamu
Ni jina lake Yesu;
Thamani na tamu
Ni jina lake Yesu.

Sasa, peleka jina la Yesu. (Kwa ajili gani?)
Liwe silaha zako. (Nini kitatendeka?)
Utakapojaribiwa,
Lilia jina hilo.

Thamani, na tamu
Ni jina lake Yesu
Thamani na tamu
Ni jina lake Yesu.

[Ndugu Branham aongea na mtu fulani katika kusanyiko—Mh.]

292 Kwa mahojiano: Billy asema mumwone kati ya sasa na Jumatano kwa mahojiano au toka Jumatano na kuendelea hadi Jumamosi kwa mahojiano yanayofuata, kama. . .Tusipokuwa na mikutano baada ya Jumatano, pangeni naye, ninyi mlio na mahojiano. Baadhi yenu, yeye hajui jinsi ya kuwapata. Kwa hivyo yeye ata. . .Wote wanaotaka mahojiano sasa, wafanye mipango na Billy.

293 Mwampenda? Vema. Sasa, hata twonane, Mungu awabariki. Tunataka kuinamisha vichwa vyetu; nami nitamuuliza rafiki yangu mwema, mwaminifu, anayeenda nchi za ng'ambo sasa, kule Afrika, ambapo wakati mmoja nilifanya kazi ya umisheni kule katika Jina la Bwana, Ndugu Sidney Jackson, yeye na mkewe. . .Tumekuwa na furaha tele wao walipokuwa pamoja nasi kwa hizi ibada chache zilizopita. Jinsi Mungu amembariki. Nami nitamwuliza Ndugu Sidney Jackson kama yeye anaweza kutufungia mkutano huu halafu tuondoke. Ndugu Jackson, tafadhali.

Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org